Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Saba - Tarehe 11 Februari, 2004**

*(Mkutano Uilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 90

**Kukosekana kwa Huduma za Kijamii - Bukombe**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. MHE. ROBERT K. MASHALA)** aliuliza:-

Kwa kuwa Watanzania waishio Bukombe wameshuhudia maendeleo makubwa yaliyotokana na kukua kwa uchumi wa Taifa kwa asilimia 6.2 mwaka 2002 kwenye Mikoa na Wilaya zingine huku Wilaya yao ikiwa haina kabisa huduma muhimu kama umeme, simu, maji, hospitali na kadhalika. Hali ambayo inawafanya waonekane hawatendewi haki na Serikali yao.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa kero hiyo?

(b) Je, Serikali katika mwaka 2003/2004 imepanga kushughulikia kero zipi kati ya hizo nilizozitaja?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Robert Mashala, Mbunge wa Bukombe, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania, *TANESCO* imekuwa na mikakati ya kuhakikisha inapeleka huduma ya umeme kwenye miji yote ambayo ni Makao Makuu ya Wilaya hapa nchi pamoja na vitongoji vya vijiji vilivyomo kwenye maeneo zinamopita *line* za umeme. Wilaya ya Bukombe imo katika mpango huo kwa nia thabiti ya kuona umeme unaangaza Mjini Ushirombo, Makao Makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, kikwazo kikubwa katika kutekeleza azma hiyo ni ukosefu wa fedha za kusaidia kugharamia miradi hiyo. Hata hivyo, Serikali imefanya juhudi za kutafuta mfadhili wa kupeleka umeme Wilayani Bukombe, *SIDA* imeonyesha nia ya kugharamia mradi huo. Mradi huo unakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 2.0. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba Serikali itapeleka umeme Bukombe mara baada ya kupata fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma ya maji, Serikali imechangia kikamilifu katika juhudi za wananchi, kuendeleza huduma hiyo hususan Mjini Ushirombo, ikiwa ni pamoja na kufufua mradi wa bomba Bwelwa.

Aidha, kwa kushirikiana na Serikali ya Uholanzi imeanzisha Programu ya Maji Vijijini na Usafi wa Mazingira unaohudumia Wilaya zote za Mkoa wa Shinyanga, ambapo wananchi huchangia 5% na Halmashauri ya Wilaya huchangiwa 5% ya gharama ya miradi. Pamoja na juhudi hizo, Serikali inaratibu mradi wa kuchimba visima unaofadhiliwa na *World Vision (T),* ambapo visima 235 vinatoa huduma Wilayani Bukombe. Visima 21 ambavyo ni vibovu vinakarabatiwa. Zoezi la uchimbaji visima virefu pia linaendelea vizuri kwa kuwashirikisha wananchi kwenye mradi wa maji na usafi wa mazingira. Wananchi wanaelimishwa na kuhamasishwa waanzishe vikundi vya watumiaji maji vinavyotambulika ili kusimamia maendeleo ya mradi, hususan uchimbaji na *pump* za visima katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba huduma za afya Bukombe bado hazitoshelezi, baadhi ya wananchi hupata huduma katika Hospitali ya Kahama. Kwa kutambua tatizo hii, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika sekta ya afya ilianza kuchukua hatua za kujenga Hospitali ya Wilaya, ili kupunguza na kuwaondolea wananchi kero. Hadi sasa, ujenzi wa jengo la huduma za akinamama na watoto *(MCH Clinic)* umekamilika na maboma matano ya wodi za kulaza wagonjwa yameezekwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2003/2004 Serikali inaandaa mpango kabambe *(Hospitali Master Plan)* wa Hospitali ya Wilaya.

Pili Wilaya inaendelea kujadiliana na Serikali ya Uholanzi kupitia Mpango wa Maendeleo Vijijini ili kupata ufadhili wa shilingi 90,867,029 kwa ajili ya kujenga majengo ya Upasuaji na Maabara na tatu Serikali Kuu imetenga jumla ya shilingi 18,000,000 kwa ajili ya kujengo jengo la wagonjwa wa nje *(Out Patient Department - OPD).*

Mheshimiwa Spika, mwisho niseme kwamba ni kweli kwa hivi sasa Bukombe hakuna huduma ya mawasiliano ya simu. Lakini Serikali kupitia Kampuni ya Simu Tanzania imefanya tathmini iliyoonyesha mwelekeo mzuri wa biashara ya simu. Kwa matokeo hayo, Bukombe imeingizwa kwenye mpango wa uboreshaji wa mawasiliano ya simu. Mpango huu utatekelezwa mwaka huu 2003/2004.

**MHE. ROBERT K. MASHALA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kuhusu matatizo ya Bukombe naomba kuuliza swali moja kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wananchi wa Bukombe wameonyesha nia yao ya kujenga Hospitali ya Wilaya na nina imani Mheshimiwa Waziri Mkuu, juzi alikuwa Bukombe ameona hatua iliyofikiwa. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kuunga mkono wananchi wa Bukombe katika ujenzi wao wa Hospitali ya Wilaya hivi karibuni? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Robert Mashala. Nawapongeza wananchi wa Wilaya ya Bukombe kwa kuamua kujiondolea kero yao na kujijengea wenyewe hospitali hiyo. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali itashirikiana nao haitawaangusha na pindi watakapo maliza ujenzi wa hospitali hiyo, Serikali itatoa huduma zote za msingi ikiwa ni pamoja na wataalam, madawa na vifaa vya hospitali kama zilivyo hospitali zingine. Pindi uwezo ukiwepo swali hilo linaweza likajibiwa baada ya muundo wa Bajeti ya mwaka huu kukamilika endapo kutakuwa na uwezo.

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea Waheshimiwa Wabunge, naomba kutambua kuwepo katika *gallery* ya Bunge letu siku ya leo kwa Mheshimiwa Balozi wa Korea ya Kusini, ambaye anamaliza muda wake. Kwa hiyo, amekuja Dodoma kwa madhumuni ya kuliaga Bunge letu rasmi kabla hajaondoka nchini.

*May I recognize the presence of the Ambassador of South Korea. You are most welcome to the House. (Makofi)*

Na. 91

**Kituo cha Afya cha Mtinko**

**MHE. MGANA I. MSINDAI (k.n.y. MHE. LAZARO S. NYALANDU)** aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Mtinko kilichopo Singida Vijijini, kina hadhi ya kuwa Hospitali kutokana na ukweli kwamba kina majengo na mitambo ya hali ya juu kupita hata hospitali ya Mkoa.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kukifanya kituo hicho kuwa hospitali?

(b) Je, ni lini Tarafa ya Mtinko itapatiwa mawasiliano ya simu ili kusaidia kuokoa maisha ya wananchi wanaohitaji huduma za dharura za ambulance ili wapelekwe hospitali?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lazaro Nyalandu, Mbunge wa Singida Vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Mtinko kinamilikiwa na Masista wa Kanisa wa Katoliki. Kituo hiki kimekuwa kikitoa huduma mbalimbali za maendeleo na kijamii kwa wananchi wa Tarafa ya Mtinko na wale watokao nje ya tarafa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa kituo hiki maombi ya kutaka kituo kipandishwe hadhi ya kuwa Hospitali yamekwishawasilishwa Wizara ya Afya, baada ya kujadiliwa na kupitishwa na ngazi ya Mkoa. Wizara ya Afya kimsingi imeyakubali maombi haya hata hivyo kabla ya kukipandisha hadhi Kituo, Uongozi wa Kituo umetakiwa kuongeza Tabibu *(Clinical Officer)* mmoja na wauguzi 50 ili kufikia idadi inayotakiwa yaani muuguzi mmoja kwa vitanda vitatu kwa kila zamu. Pia vyeti vya kitaaluma kwa wafanyakazi wote wahusika vimetakiwa kuthibitishwa.

(b) Maombi ya kufunga simu kwenye Tarafa ya Mtinko yamewasilishwa katika Kampuni ya Simu Mkoa wa Singida na tathmini ya kibiashara imefanyika na kuwasilisha taarifa Makao Makuu Dar es Salaam.

Matarajio ni kwamba kama tathmini hiyo ikipitishwa, mradi huu utaingizwa kwenye mpango wa kampuni wa mwaka 2004. Nawaomba Wakazi wa Tarafa ya Mtinko wawe na subira wakati kampuni inayafanyia kazi maombi haya.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niulize swali moja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile sasa hivi nina uhakika hiyo kazi ya kuongeza watalaam aliosema Naibu Waziri imeshafanyika. Sasa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa umefika wakati wa kukipandisha kile Kituo cha Afya kipate hadhi ya hospitali kamili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Msindai, kama ifuatavyo:-

Kama kweli kwamba idadi ya wafanyakazi waliotakiwa na Wizara ya Afya imeshapatikana basi nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mgana Msindai, kwamba hadhi ya Kituo hicho kuwa Hospitali itapandishwa mara moja.

Na. 92

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Mji wa Kibao - Mufindi**

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji Mdogo wa Kibao Wilayani Mufindi ulikuwa Mji Mkuu wa Wilaya ya Mufindi hadi mwaka 1975 Makao Makuu yalipohamia Mafinga na kwa kuwa Mji huo umezungukwa na mashamba makubwa ya chai na vijiji vyenye wakazi wengi vya Sawala, Mtwango, Mpunga, Lufuna, Kitiru, Itukili, Mninga, Kihanga, Mkalala na kadhalika lakini hakuna Kituo cha Afya;

(a) Je, Serikali haioni kwamba imechelewa sana kujenga Kituo cha Afya katika kijiji ambacho kuna Zahanati ndogo tu?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani sasa ya kujenga Kituo cha Afya - Kibao hasa ikizingatiwa kuwa vijiji husika na Makampuni yaliyoko kwenye maeneo hayo wanazalisha zaidi ya asilimia 50 ya chai yote nchini na kuliingiza Taifa mapato makubwa?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, Mbunge wa Mufindi Kusini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia sera ya afya, kituo cha afya kimoja kimekadiriwa kutoa huduma kwa watu 50,000 au wakazi wa Tarafa. Mji wa Kibao upo katika Kata ya Mtwanga yenye wakazi 18,242. Kata hii ipo katika Tarafa ya Ifwagi ambayo ina kituo cha afya cha Ifwagi.

Vijiji vingine alivyovitaja Mheshimiwa Mbunge vya Ilukilu, Kihanga na Mkalala vipo katika Kata ya Kasanga, Tarafa ya Kasanga ambayo pia ina Kituo cha Afya cha Kasanga kilichopo umbali wa Km. 18 kutoka Kibao.

Vilevile kuna jumla ya Zahanati 4 na Hospitali ya Lugoda inayomilikiwa na Kampuni ya Chai ya *Brooke Bond* iliyoko umbali wa kilometa 4 toka Mji Mdogo wa Kibao. Hivyo kwa misingi ya maelezo haya kwa sasa hakuna sababu za kujenga kituo cha afya katika Mji Mdogo wa Kibao. Serikali itaimarisha na kuboresha zaidi huduma zinazotolewa na Zahanati ya Kibao kupitia programu zinazotekelezwa chini ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia mipango ya Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi.

(b) Mheshimiwa Spika, kulingana na vigezo vya kujengwa kwa kituo cha afya, kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga kituo kipya cha afya katika Mji Mdogo wa Kibao kwa kuwa kipo Kituo cha Afya cha Ifwagi katika Tarafa ya Ifwagi umbali wa kilometa 18 kutoka Zahanati ya Kibao. Aidha, kuna Hospitali ya Lugoda inayohudumia Watumishi wa Kampuni ya Brooke Bond na wananchi waishio jirani nayo na zipo zahanati nne zinazohudumia wananchi wa eneo hili.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri nina swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wilaya ya Mufindi ina jumla ya wakazi 284,000 na kwa kuwa Wilaya ina vituo vitatu tu vya afya, nikimaanisha kwamba kituo kimoja kinahudumia zaidi ya wananchi 90,000.

(a) Je, haoni utaratibu unaotumika kwa sasa wa kutafuta umbali kwamba kiko kilometa 18 na kwa maana hiyo hakina sifa ya kupata kituo cha afya ni utaratibu ambao umepitwa na wakati? *(Makofi)*

(b) Baada ya swali langu la (a) haoni iko sababu ya mimi mwakilishi wa wananchi wa Mufindi tukae na Wizara ya Afya, ili tutatue tatizo hili kwa sababu kwa majibu yake itaonyesha kwamba Wilaya ya Mufindi itabaki na vituo vitatu tu kuhudumia wakazi 284,000 kwa miaka yote?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu la Mheshimiwa Benito Malangalila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haiangalii au haipigi hesabu ya umbali wa kituo kimoja hadi kingine. Isipokuwa kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi inaangalia vigezo viwili, inaangalia idadi ya watu wanaohudumiwa na kituo sasa kwa hesabu za Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba hajaingiza mahesabu kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya. Kama unavyofahamu idadi ya watu ni jambo moja na la pili, ni kuwepo kwa hospitali ya Wilaya. Katika tarafa ambayo Hospitali ya Wilaya ipo haiwezekani tena ukaweka kituo cha afya kwa sababu Hospitali ya Wilaya, itakuwa inahudumia wananchi wale.

Kwa hiyo, napenda kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba hesabu alizozipiga lazima aelewe kwamba Hospitali ya Wilaya nayo inatoa huduma kwa wananchi wa hapo.

Kuhusu Mheshimiwa Mbunge kukaa na Wizara ya Afya kujadili hili, mimi niko tayari kukaa naye ili tumpe maelekezo zaidi ambayo yataweza kumsaidia kupata ufumbuzi wa jambo hili. Napenda nimshauri Mbunge kwamba kama kuna tarafa ambayo haina kituo cha afya hiyo ndiyo hoja ya kuweka badala ya kuweka idadi ya Wilaya nzima kwa ujumla bila kuweka maanani huduma zinazotolewa na Hospitali ya Wilaya. *(Makofi)*

Na. 93

**Madaktari Bingwa Hospitali ya Mkoa Singida**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Singida haina Madaktari Bingwa wa fani za upasuaji, magonjwa ya wanawake na watoto:-

(a) Je, Serikali inalifahamu tatizo hilo?

(b) Kama Serikali inalifahamu tatizo hilo je, imeweka mikakati gani ya haraka ya kunusuru maisha ya wananchi wa Mkoa wa Singida na vile vile kuwapunguzia adha na ghasia za usafiri kwenda hospitali za rufaa kufuata huduma?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati najibu swali namba 82 la Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini wakati wa Bunge la Mkutano wa Bajeti ya mwaka 2002/2003. Serikali inalifahamu tatizo hili la kutokuwepo kabisa Madaktari Bingwa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida. Kwa mujibu wa muundo wa ikama ya Watumishi wa sekta ya afya, Hospitali ya Mkoa wa Singida yenye vitanda 350 inastahili kuwa na Madaktari Bingwa sifa katika fani za upasuaji, magonjwa ya watoto, magonjwa ya macho, magonjwa ya akili, uzazi na wanawake na magonjwa ya kawaida.

(b) Mheshimiwa Spika, kuanzia mwaka wa fedha wa 2000/2001 hadi sasa Mkoa umekuwa ukiomba ikama ya Madaktari Bingwa hao sita na Serikali wakati wote imekuwa ikiidhinisha nafasi hizo na kuzitengea fedha za mishahara katika Bajeti ya Mkoa. Tatizo linalojitokeza kila mwaka ni kutopatikana kwa wataalam hao kutokana na upungufu uliopo Kitaifa. Kuondokana na tatizo hili Mkoa wa Singida

umeahidiwa kupata Madaktari Bingwa watatu kutoka Cuba kufuatia Mkataba wa Ushirikiano uliosainiwa kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali Cuba.

Kama ufumbuzi wa muda, Serikali imekuwa ikipeleka madaktari wasio mabingwa lakini wenye uzoefu wa kazi kila inapowezekana ili kukabiliana na tatizo la upungu mkubwa wa madaktari Bingwa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida. Kwa sasa hospitali hii inao madaktari wa kawaida watano kati ya 10 wanaohitajika, madaktari wasaidizi na Daktari Msaidizi *AMOs - A naesstetist* mmoja.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa majibu mara kadhaa katika Bunge hili Tukufu kuletewa madaktari Mkoa wa Singida lakini imekuwa ni ahadi ambazo hazitekelezeki.

(a) Je, haioni kwamba kuna haja ya kuwa na muda maalum ambao utatekelezeka ili angalau wananchi wa Mkoa wa Singida wajenge imani na Serikali? *(Makofi)*

(b) Kwa kuwa Mkoa wa Singida una wananchi kama mikoa mingine kwa nini Serikali haioni umuhimu kuwa mgao unaofanana na mikoa mingine kuliko ilivyo sasa mikoa mingine ina madaktari wengi na wakati Mkoa wa Singida hauna? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA (k.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI YA MITAA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Diana Chilolo, kama ifuatavyo:-

Ahadi iliyotolewa ya madaktari wa Cuba kupelekwa katika Hospitali ya Mkoa wa Singida itatekelezwa hivi karibuni. Kama unavyofahamu tumewekeana mkataba na wenzetu wa Cuba, madaktari ambao tayari wameshapatikana kule kwa kuja Tanzania ni 50 kati ya 70 walioombwa. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba wakifika madaktari hao basi kama tulivyoahidi madaktari 3 watapelekwa Singida. *(Makofi)*

Kuhusu la mgao unaofanana katika Mikoa napenda kusema kama ifuatavyo:-

Sasa hivi utaratibu ni kutoa vibali vya ajira na kama nilivyosema katika jibu la msingi ni kwamba vibali vya ajira kwa ajili ya Madaktari Bingwa wa Mkoa wa Singida vimetolewa na mishahara yao imetengwa katika Bajeti ya Mkoa. Tatizo ni kwamba wanapotangaza nafasi hizo Madaktari Bingwa kwa kuwa ni wachache wanakuwa hawajitokezi kwenda Mkoa wa Singida.

Kwa hiyo, kwa kutambua hilo Serikali sasa inapanga utaratibu wa kuwapeleka hao madaktari wa kutoka nje Mkoa wa Singida na vile vile tunaangalia uwezekano wa kuweka posho maalum kwa ajili ya Mikoa ambayo ina uhaba wa madaktari. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHEGENI R. MASUNGA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa kumekuwa na vijana wengi wa Kitanzania wanaohitimu katika fani mbalimbali na hasa udaktari wanakwenda nje ya nchi kufanya kazi kwa sababu wanapata maslahi duni hapa nchini. Je, isingekuwa vema kwa Serikali kuboresha hii fani ya madaktari waweze kupata malipo ambayo yatawawezesha kufanya kazi hapa nchini, badala ya kukimbilia nje? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Chegeni Raphael Masunga, baada ya majibu mazuri yaliyotolewa na Naibu Waziri wa Afya kwa niaba ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwamba ni kweli kabisa watalaam ni wachache sana wakiwemo wale afya na hasa ukizingatia kwamba sekta binafsi na nchi nyingine zinalipa zaidi. Lakini ningependa kusema kwamba kupitia zoezi na tathmini ya kazi Idara ya Utumishi imejaribu

kuona ni namna gani iweze kuwamotisha watalaam wale ambao ni wachache na huduma zao ni nyeti ili waweze kubakia ndani ya nchi, badala ya kwenda kutafuta kazi mahali pengine.

Lakini naomba nikumbushe kwamba tunaweza tukalipa watalaam wetu vizuri kutokana na bidii ya kazi na kuongeza tija ndani ya nchi pamoja na mambo mengine ambayo tunayafanya ili kuwamotisha watalaam wetu. *(Makofi)*

Na. 94

**Hospitali ya Rufaa kwa Mikoa ya Kusini**

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO (k.n.y. MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ)** aliuliza:-

Kwa kuwa Mikoa ya Kusini mwa Tanzania yaani Lindi na Mtwara hakuna Hospitali ya Rufaa;

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia Mikoa hiyo Hospitali ya Rufaa?

(b) Je, ni lini mradi wa ujenzi wa hospitali ya aina hiyo utaanza na kukamilika?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz ,Mbunge wa Lindi Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haijabadili azma yake ya kuipatia Mikoa ya Lindi na Mtwara Hospitali ya Rufaa kwa nia ya kupanua, kuimarisha na kuboresha huduma za afya nchini. Tatizo la kujenga Hospitali hiyo ya Rufaa ni ukosefu wa fedha. Nilizungumza katika Bunge lako Tukufu mwezi Aprili, 2002 kuwa Serikali kupitia Wizara yangu ilifanya mazungumzo ya Serikali za China na Uingereza kuhusu ujenzi wa hospitali, hiyo lakini walishindwa kutusaidia kutokana na ukubwa wa gharama. Serikali ya Japan, bado inaangalia uwezekano wa kutusaidia kujenga Hospitali ya Rufaa. Endapo Serikali ya Japan itakubali kutusaidia Bunge lako tukufu litaarifiwa. Ninamuomba Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, kwa niaba ya wananchi wote wa Lindi na Mtwara wavute subira.

(b) Mheshimiwa Spika, ni vigumu kuzungumza kwa uhakika kuwa ujenzi wa Hospitali hiyo ya Rufaa utaanza lini kwa vile hatuna fedha za kujenga hospitali hiyo kwa sasa. *(Makofi)*

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, ningependa kujua hakuna mpango unaoweza ukafanywa kwa kushirikiana na Hospitali ya *Mission* iliyoko Nyangao au Ndanda kwa kipindi hiki ambacho hatuna Hospitali ya Rufaa tukaweza tukazitumia hospitali hizo kama mojawapo katika Hospitali za Rufaa kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hassan Chande Kigwalilo, kuwa kushirikiana na Hospitali za *Mission* utaratibu huo unawezekana, lakini kinachotakiwa ni kutimizwa kwa vigezo vya Hospitali ya Rufaa. Jambo hilo limefanyika katika Hospitali ya *KCMC* na Hospitali za Bugando ni hospitali za *Mission* wameingia mkataba na Serikali, lakini wametimiza vigezo vivyotakiwa kwa Hospitali za Rufaa. Kwa hiyo, endapo kuna shirika lolote la kidini ambalo liko tayari kushirikiana na Serikali katika kujenga hospitali ya rufaa, Wizara yangu itakuwa tayari kushirikiana nao. *(Makofi)*

**MHE. ABDILLAHI O. NAMKULALA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa ujenzi wa hospitali ya rufaa mpya ni gharama kubwa. Je, haiwezekani kufanya ukarabati na kuongeza majengo katika Hospitali ya Ligula ikapandishwa ikawa ya rufaa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA AFYA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdillahi Namkulala, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema Hospitali ya Rufaa ina vigezo vyake, inatakiwa iwe na wodi zinazotakiwa, maabara ya kisasa, chumba cha *X- Ray* chenye hadhi ya Hospitali ya rufaa na Madaktari Bingwa na kadhalika. Sasa endapo hospitali yoyote itaweza kushirikiana na Serikali katika kupata hadhi ya Hospitali ya Rufaa kama nilivyosema awali, Wizara yangu haitasita kushirikiana nao ili kuifanya Hospitali ya Rufaa. Sasa sina uhakika kama hospitali hii ina hadhi kama hiyo. Lakini endapo tutaona kwamba wana uwezo wa kuifikisha hadhi ya Hospitali ya Rufaa basi tutaweza kushirikiana nao. *(Makofi)*

Na.95

***Organic Farming***

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA (k.n.y. MHE. ROSEMARY H. NYERERE)** aliuliza:-

Kwa kuwa inasemekana kwamba *Organic Farming* inaweza kutoa mazao ambayo ni bora zaidi kwa matumizi ya binadamu na ardhi na kwa kuwa hata bidhaa zinazotokana na *Organic Farming* zinauzwa kwa bei ya juu zaidi hususan kwenye Soko la Kimataifa:-

(a) Kama kweli *Organic Farming* inayo manufaa; Je, Serikali inaweza kuelezea manufaa hayo?

(b) Je, mafunzo ya *Organic Farming* yanatolewa wapi katika Jiji la Dar es Salaam na wananchi wanaoweza kuyapataje? Je, Serikali ina mpango gani wa kusambaza elimu hiyo kwenye sehemu nyingine nchini nje ya Jiji la Dar es Salaam?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuanzisha kilimo cha aina hiyo katika miradi ya umwagiliaji ya Bugwema, Butiama na maeneo mengine ya Mkoa wa Mara yenye vyanzo vya Maji vya uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Huria Kambarage Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, kwanza napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Kilimo hai *(Organic Farming)* ni utaratibu wa kuzalisha mazao bila kutumia madawa ya viwandani na kuulia wadudu au mbolea za chumvi chumvi kwa maneno mengine bila kutumia *Inorganic Chemicals*. Katika nchi zilizoendelea, wapo watu awmboa wanapendelea kutumia mazao yanayotokana na kilimo hai na wako tayari kulipa bei kubwa kwa mazao hayo kwa madai kwamba ni mazuri kwa afya zao na kilmo hicho hakiharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rosemary Huria Kambarage Nyerere, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Manufaa ya kilimo hai yanategema yanatazamwa kutoka upande gani? Walaji wanakiona kuwa na manufaa kwa afya zao, wakati wazalishaji wanapata manufaa ya kuhifadhi mazingira kupata solo la uhakika na pengine kupata bei nzuri kwa mazao hayo.

Kuna haja ya kuchukua tahadhari kwa kuwa katika maeneo mengi mazao yanayoweza kupatikana kwa eneo kutokana na kilimo hai yanaweza kuwa machache kulimo yale ambayo yangeweza kupatikana kwa kutumia kemikali za viwandani. Inabidi kupima manufaa yanayopatikana kwa kuangalia gharama na mapato ya kila utaratibu wa uzalishaji.

Aidha, kilimo hai hakiwezekani kwa mazao yanayolimwa kwenye mashamba makubwa. Kwa mfano, miwa au kwenye maeneo ambayo udongo umepoteza virutubisho kwa wingi kama ilivyo kwenye Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

(b) Hakuna mahali maalum ambapo mafunzo ya kilmo hai yanatolewa kwenye Jiji la Dar es Salaam. Mafunzo maalum kwa wakulima yanaweza kuandaliwa na kutoelwa pale yanapohitajika. Aidha, Maafisa Kilimo wanaoweza kutoa ushauri wa mbinu za Kilimo hai katika maeneo hayo.

(c) Serikali iko tayari kuwafundisha wakulima wa miradi ya umwagiliaji ya Bugwema, Butiama na maeneo mengine ya Mkoa wa Mara mbinu za kilimo hai. Napenda kusisitiza kwamba sehemu kubwa sana ya kilimo chetu ni *organic.* Maeneo mengi ya nchi hayatumii mbolea za chumvi chumvi wala madawa ya kuulia wadudu.

Kitaifa tunatumia mbolea kidogo sana. Inakisiwa kwamba tunatumia wastani wa kilo sita tu za mbolea kwa hekta na kwamba tunaondoa wastani wa kilo 90 za virutubisho kwa mwaka kwa hekta na kurudisha kilo tisa tu. Katika maeneo mengi ya nchi, kilimo hakiwezekani bila mbolea. Malengo yetu ni lazima yawe kuongeza matumizi ya mbolea ili kuongeza uzalishaji ili kujihakikishia upatikanaji wa chakula na kuondoa umasikini. Kilimo hai kitahimizwa kwa mazao maalum na kwa masoko maalum na siyo badala ya kilimo cha kutumia mbolea na madawa.

**MHE. IBRAHIMU W. MARWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula, nilikuwa napenda kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Waziri amekiri katika maelezo yake kwamba kuna maeneo katika nchi yetu ambayo bado kilimo hiki cha kutokutumia mbolea kinaweza kufanyika na kwa manufaa; je, Waziri haoni kwamba kuna umuhimu wa kuya-*identify* maeneo hayo na wananchi wakasaidiwa kuimarisha kilimo cha namna hiyo ambacho kina faida nyingi zaidi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, mazao hayo ya kilimo hai yanaweza kufanyika popote nchini, ni uamuzi. Yanaweza kufanyika huko anakotoka Mheshimiwa katika Mkoa wa Mara au inaweza kufanyika hata hapa Dodoma. Kinachotakiwa tu ni kutambua ni mazao gani yanafaa katika ardhi ile, lakini yanaweza kufanyika popote. Ni kutokutumia kemikali. Unatumia mbolea ambazo sio za kemikali kwa mfano samadi, mboji na kadhalika. Hiyo ndiyo maana ya kilimo hai. Kutokutumia madawa. Kama ni mbolea au madawa ya kuzuia wadudu ambayo siyo ya kemikali, hicho ndio kigezo cha kilimo hai. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu la msingi Naibu Waziri amesema kuwa matumizi ya mbolea ya kemikali ni kidogo sana na kwa kweli kwa taarifa zilizopo ni kwamba imepungua kutoka kiwango ambacho kiliwahi kutumika siku za nyuma, na kwa kuwa ili kuweza kuzalisha kwa wingi kama alivyosema yeye mwenyewe kwenye jibu lake, ni kwamba lazima matumizi ya mbolea yaongezeke, na kwa kuwa matumizi ya mbolea sio suala la kuagiza mbolea tu ndani ya nchi, ni masuala ya matumizi

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuamsha ari (ku-*stimulate)* matumizi zaidi ya mbolea hizi za *organic* ili kuongeza uzalishaji katika nchi yetu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, wanaohusika na ku-*stimulate* au kuhakikisha kama kuna kilimo hai ni hao hao Maafisa wa Kilimo. Kwa hiyo, kama unataka kilimo maalum kwa soko maalum, maana unaweza kulima usipate soko kwa mazao fulani fulani. Kwa hiyo, itabidi ujadiliane na wataalam wetu wa kilimo kuonesha ni kitu gani unataka kiwe katika kilimo hicho hai. Kwa mfano, unasema mboga mboga na kama ni mboga ni aina gani na soko liko wapi. Sasa tutaangalia jinsi ya kuzalisha hizo mboga bila kutumia mbolea za kemikali.

Aidha, sasa hivi tunasema Tanzania bado kilimo chetu kama ni mali hai kwa sababu matumizi ni kidogo sana. Ulaya wanatumia kwa hekta moja karibu mifuko kama mitano hivi kwa hekta moja. Sisi

tunatumia kilo sita. Kwa hiyo, tunahitaji kwanza kuongeza matumizi kufikia kiwango kile kinachoweza kusaidia tija katika kilimo, lakini papo hapo wanaotaka soko la kilimo mali hai, basi ni kuzungumza na wataalam wetu wa kilimo hapo ulipo.

**SPIKA:** Tunaendelea. Maswali kwa Meja Mstaafu Makundi, hayupo. *Chief Whip* wa Upinzani mwulizie swali lake.

Na. 96

**Maafisa Kilimo katika Ngazi zote**

**MHE. THOMAS NGAWAIYA (k.n.y. MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI)** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka mingi sasa kumekuwa hakuna Maafisa Kilimo Tarafa, Kata, Kijiji na hivyo wakulima Vijijini hulima, hupanda, hutumia mbolea kwa utashi wao wenyewe hasa kwa zao la kahawa ambalo miti mingi huko Vijijini ina umri wa zaidi ya miaka 80 na mkulima huyo hana utaalamu wala uwezo wa kuboresha miti hiyo tena:-

(a) Je, kuna haja gani ya kuwa na Wizara ya Kilimo na Chakula? Je isingefaa sehemu ya kilimo ikafutwa ikabakia Wizara ya Chakula peke yake?

(b) Je, kama Wizara hiyo itaendelea kubaki madarakani, ina mpango gani wa kuwadhibiti kinidhamu ya utendaji kazi kwa walioajiriwa kama Maafisa Kilimo kwenye ngazi nilizotaja ili kufufua mazao hayo yanayotetereka na kupoteza fedha nyingi za kigeni kila mwaka?

(c) Je, Waziri na Naibu wake wanayo ratiba yoyote ya kutembelea mashamba ya Vijiji kadhaa hapa nchini ili kujionea kwa macho yao wenyewe udhaifu wa hao Maafisa Kilimo wa ngazi hizo pamoja na wakulima ambao wanatumia utashi wao kwa shughuli za kilimo bila ushauri wa wataalam hao wa kilimo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa *Major* Mstaafu Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Wakati wote wakulima wataendelea kuzalisha mazao kwa utashi wao kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu watakaopewa.

Wilaya zote za Tanzania zina wataalam wa ugani katika ngazi mbalimbali za utawala. Kwa mfano, Wilaya ya Moshi Vijijini ambayo ina Vijiji 165, Kata 31 na Tarafa nne, ina bahati ya kuwa na Maafisa ugani 181 ambao wakipangwa vizuri watawezesha kila Kijiji kuwa na mtaalam mmoja wa ugani. Hadi tarehe 19 Janauari, 2004, Wilaya ya Moshi Vijijini ilikuwa na wataalam 106 katika Vijiji, 56 kwenye Kata na 16 kwenye Makao Makuu ya Wilaya. Hivyo si kweli kuwa hakuna Maafisa Kilimo katika Kata na Vijiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Major* Mstaafu Jesse Makundi, Mbunge wa Vunjo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Kazi za Wizara ya Kilimo na Chakula zimefafanuliwa kwenye hati iliyoanzisha Wizara hiyo. Huduma za ugani ni moja tu ya kazi nyingi za Wizara. Kazi nyingine ni pamoja na kutunga sera za kusimamia utekelezaji wake, kupanga matumizi bora ya ardhi kwa ajili ya kilimo, kuendeleza utafiti wa kilimo, kusimamia hifadhi ya chakula na ujenzi wa maghala, kuendeleza raslimali watu katika Sekta na kuratibu Taasisi na wakala wa asasi zilizoko chini ya Wizara.

(b) Ili kuboresha huduma za utoaji utaalamu wa kilimo na mifugo kwa wakulima, wataalamu waliopo katika ngazi za Wilaya hadi Vijijini walihamishiwa kwenye Serikali za Mitaa tangu mwaka 1998. Lengo la uamuzi huo ni kuwaweka watalaam karibu na wakulima ili wasimamie uzalishaji wa kilimo na

mifugo kwa karibu zaidi kuliko ambavyo ingekuwa kama wangeendelea kuwa moja kwa moja chini ya Wizara. Halmashauri za Wilaya au Miji, ikiwa ni pamoja na wakurugenzi Watendaji, Madiwani na Wabunge, wanalo jukumu la kuwapangia kazi, kuwasimamia na kudhibiti nidhamu ya kazi. Kazi ya Wizara ni kuandaa miongozo ya kitaalamu na kuisambaza Wilayani, kuwapatia Maafisa Ugani mafunzo na matokeo ya tafiti mbalimbali na kushirikiana na TAMISEMI na Tume ya Utumishi katika Serikali za Mitaa juu ya maendeleo na matumizi bora ya Maafisa hao.

(c) Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa tunazo ratiba za kazi. Mojawapo ya kazi hizo ni kutembelea Miko ili kutoa ushauri na maagizo ya kutatua matatizo yanayokikabili kilimo. Hadi mwezi wa Januari, 2004, tumekwishatembelea karibu Mikoa yote ya Tanzania Bara. Narudia kusisitiza kwamba jukumu la kuwasimamia Maafisa Kilimo walioko Vijijini ni la Halmashauri za Wilaya na Vijiji vinavyohusika.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Naomba nimwulize Mheshimiwa Naibu Waziri; kwa kuwa katika suala la msingi linazungumzia mibuni ambayo imezeeka yenye miaka zaidi ya 80 na kwa kuwa kunahitajika miche mipya ili kuboresha na kwa kuwa tumepeleka shilingi bilioni 12 katika Kituo cha Lyamungo kwa ajili hiyo; je, Serikali haioni kuwa ni busara sasa kutoa miche hiyo kwa wingi na bure kwa wananchi wa Kilimanjaro?

Pili, kwa kuwa katika suala la msingi linazungumzia Maafisa Ugani *(Extension Officers)* na kutokana na jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri ni kwamba wako wengi; je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwamba hao Maafisa Ugani hawaonekani katika maeneo husika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mibuni imezeeka. Tuliona hivyo tulipotembelea Kituo cha Utafiti cha Takri kule Kilimanjaro nikiwa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Ardhi. Jitihada inafanyika kuzalisha miche kwa wingi kwa kati ya miche kama milioni saba kwa mwaka kuisambaza nchi nzima, sio Kilimanjaro peke yake, ni Mikoa yote kunakolimwa kahawa, iwe Bukoba, Ruvuma, Morogoro na kadhalika. Hapo hapo zinatumika hela kuona kama kuna uwezekano wa kutumia vikonyo kwa shughuli hiyo. Kasi ipo na jitihada ipo, tuliona miche ambayo imeandaliwa kwa shughuli hiyo tulipotembelea Kituo kile cha Lyamungo na Mheshimiwa Thomas Ngawaiya.

Sasa kuhusu Maafisa Ugani, wapo wengi hawaonekani; wapo na inawezekana kuonekana kwa sababu wako chini ya *DED,* ninachomshauri Mheshimiwa kama anapenda kuzungumzia nao, amwone *DED,* Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilimanjaro, atawaita wote awahutubie na kuwahamasisha. Nafasi ipo na ninamkaribisha na akiniita hata mimi nitashiriki. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Tunaendelea na maswali kwa Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, swali linalofuata.

Na.97

**Sera ya Usambazaji Umeme Vijijini**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Sera ya Serikali ya kusambaza umeme Vijijini imeonekana kuwa ni gharama kubwa na kwa kuwa ili kurahisisha usambazaji wa umeme Vijijii Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* limekuwa likitumia umeme wa gridi katika Mikoa inayopitiwa na umeme huo ili kuvipatia Vijiji umeme wa uhakika:-

(a) Je, Serikali imeweka mikakati gani ili kuwa na Mfuko maalm wa fedha utakaoshughulikia usambazaji wa umeme Vijijini kwa uhakika zaidi?

(b) Kwa kuwa Jimbo la Kalambo limepitiwa na umeme wa gridi toka Mbala, Zambia na maombi ya kuteremsha umeme katika Vijiji vya Kusesya, Sopa, Matai Msanzi na Kasanga haujawa na matumaini yoyote kwa Serikali licha ya juhudi zangu kuwaona wahusika wa ngazi zote; je, ni lini umeme utapatikana katika Vijiji vya Kasesya, Sopa, Matai, Msanzi Kasanga na Mwimbi?

(c) Je, Serikali haioni kwamba kutopeleka umeme Jimboni Kalambo ni kutaka wananchi wa Jimbo hili wasipate maendeleo ya haraka na hivyo kubakia kuwa wasindikizaji wa maendeleo badala ya kuwa washiriki wa maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa msaada wa Serikali ya Sweden kupitia Shirika lake la Misaada la *SIDA* imeandaa taratibu za kuanzisha Mfuko maalum wa kugharamia miradi ya kupeleka nishati bora Vijijini yaani *Rural Energy Fund.* Uanzishwaji wa Mfuko huu maalum ambao unategemewa kukamilika mwaka huu 2004 utatumika pia kwa ajili ya kuyapatia umeme maeneo ya Vijijini badala ya kutegemea utaratibu wa sasa.

(b) Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Matai, Sopa, Msanzi, Katuka, Bandari ya Kasanga, Mwimbi na Kasesya vinaweza kupatiwa umeme kwa kutumia *transformer* maalum zitakazofungwa moja kwa moja katika laini ya msongo wa *66KV* kutoka Mbala hadi Sumbawanga. Hata hivyo, kutokana na Shirika kukabiliwa na ukosefu wa fedha, mpango wa kuvipatia umeme Vijiji vilivyotajwa na Mheshimiwa Mbunge utatekelezwa hali ya fedha itakapokuwa nzuri.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali daima imekuwa ikijitahidi kuhakikisha kuwa sehemu mbalimbali za nchi zinapatiwa umeme kwa kadri ya fedha zitakavyokuwa zinapatikana. Serikali kwa sasa hivi kama tunavyofahamu, inajitahidi kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya na maeneo mengine ambayo yanapitiwa na njia au miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kalambo litaandaliwa kupatiwa umeme baada ya upatikanaji wa fedha. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa Serikali imetambua umuhimu wa kilimo katika Mkoa wa Rukwa na hasa katika Wilaya ya Sumbawanga na ili tuweze kufanikisha kilimo tunahitaji nguvu za umeme ili kufanya usindikaji wa mazao, tunashukuru Wizara ya Kilimo angalau imetambua hilo, lakini Wizara ya Nishati na Madini bado inazungumza habari ya kupatikana fedha hizo; hizo fedha zitapatikana lini ili umeme usaidie kusindika mazao hayo ili kuyaongezea thamani?

Swali la pili, Wilaya ya Sumbawanga Vijijini...

**SPIKA:** Uliza swali, usiendelee na maelezo marefu marefu. Uliza swali moja kwa moja.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Swali la pili, je, Wizara ya Nishati na Madini inakubaliana nami kwamba ili kusambaza umeme katika Jimbo la Kwela na Jimbo la Sumbawanga, Matai ndipo mahali palipo katikati ili kuweza kuwafikishia wananchi umeme katika Vijiji vya Laela, Hui....

**SPIKA:** Sawa sawa. Matai ndio katikati. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, mimi nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa umeme katika kuleta maendeleo na ndio maana Serikali

imekuwa ikijitahidi katika kuhakikisha kwamba usambazaji wa umeme nchini unakwenda kwa kasi kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Matai kuwa katikati na kwamba pawe ndiyo mahali pa kuanzisha usambazaji wa umeme kwa maeneo mengine, suala la usambazaji wa umeme unaendana na taaluma ya usambazaji wa umeme na kwa kweli ni vizuri tungeliacha suala hili kwa wataalam, wakati utakapofika wa kusambaza umeme waone ni mahali gani ambapo ni katikati na ambapo ni nafuu kwa ajili ya usambazaji umeme kunakoweza kufikisha umeme katika maeneo yote. Sipingi umuhimu wa Matai lakini nadhani suala hili tuwaachie wataalam.

Na.98

**Kuunda Mamlaka ya Umeme wa Gesi ya Songo Songo**

**MHE. RAYNALD A. MROPE** aliuliza: -

Kwa kuwa hali ya kupatikana kwa umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara siyo ya uhakika; na kwa kuwa Serikali katika Mkutano wake wa Bajeti 2003/2004 ilieleza kuwa tatizo la umeme kwenye Mikoa hiyo ni mambo mawili tu yanayoweza kufanyika ambayo ni ama kuwa na Stesheni ndogo Somanga Funga ili kuzalisha umeme utokanao na Gesi ya Songosongo au kuzalisha umeme kutokana na gesi ya *Mnazi Bay:-*

(a) Je, kwa nini Serikali isianzishe Mamlaka *(Authority)* maalum ya kushughulikia chanzo cha umeme wa gesi ili uweze kusambazwa kwenye maeneo mbalimbali ya Ukanda wa Maendeleo ya Kusini badala ya kutegemea *TANESCO* ambayo uendeshaji wake umebinafsishwa?

(b) Je, Serikali haioni kwamba kuwepo na Mamlaka hiyo kutaleta ushindani na *TANESCO* hivyo kufanya huduma na bei kuwa nzuri zaidi kwa wateja kuliko kuendelea na ukiritimba wa *TANESCO?*

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuitumia ipasavyo Gesi ya *Mnazi Bay* ili licha ya kutoa umeme kwa ajili ya Ukanda wa Maendeleo Kusini, lakini pia kusaidia kupanua soko la ajira?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald Mrope, Mbunge wa Masasi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, jukumu la kusambaza umeme nchini kwa sasa ni jukumu la Shirika la Ugavi wa Umeme yaani *TANESCO. TANESCO* tangu ianzishwe mwaka 1964 imefanya kazi hiyo vizuri kulingana na makusudio yake. Hivi sasa Serikali inafanya matayarisho ya kuirekebisha *TANESCO* kwa lengo la kuongeza ufanisi, kuingiza mitaji mipya kutoka kwa wawekezaji binafsi na kuharakisha usambazaji wa umeme nchini.

Katika kurekebisha Sekta ndogo ya umeme, yanatarajiwa kuundwa Makampuni kadhaa ya kuzalisha na kusambaza umeme. Kati ya Makampuni hayo, yapo yatakayotumia gesi kama chanzo cha kuzalisha umeme. Kutokana na hayo, hakutakuwa na haja ya kuunda Taasisi maalum kwa hivi sasa kushughulikia chanzo cha umeme wa gesi wa Ukanda wa Kusini.

(b) Mheshimiwa Spika, ni nia ya Serikali kuligawa Shirika la *TANESCO* katika sehemu ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme ili kuweka mazingira ya ushindani baina ya Makampuni yatakayoundwa ili kuongeza ufanisi kama nilivyosema awali, tija na kuharakisha usambazaji wa umeme sehemu nyingi ambazo hazina umeme. Kwa kuwa tayari mkakati huo upo na Serikali imenza kuufanyia kazi, hakuna haja ya kuunda Mamlaka maalum kushughulikia umeme sehemu za Kusini kwa kuwa kwa kufanya hivyo kunaweza kuathiri hatua za kurekebisha Sekta ndogo ya umeme kwa ujumla.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali imeingia Mkataba wa Makusudio yaani *Agreement of Intent* na Kampuni ya *Artumas Group Inc.* ya Canada. Chini ya Mkataba huo, Kampuni ya *Artumas Group Inc.,* itafanya kazi ya kutathmini kiasi cha gesi iliyopo katika eneo la *Mnazi Bay* na endapo itathitibika kuwa kuna gesi ya kutosha kama ambavyo ilifahamika hapo awali, basi wawakezaji hao watajenga mitambo ya kuzalisha umeme na kuimarisha mfumo wa usambazaji wa umeme sehemu za Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Aidha, kama itapatikana gesi nyingi zaidi, wawekezaji hao wameahidi kutafuta soko zaidi la gesi kwa kuangalia uwezekano wa kuzalisha *Synthetic Fuel* kwa ajili ya matumizi ya vyombo vya usafiri, kuzalisha mbolea ya chumvi chumvi au kujenga mtambo mkubwa zaidi wa kuzalisha umeme na kuuza umeme wa ziada sehemu za Kaskazini mwa Msumbiji. Hatua hizo zitasaidia kuinua uchumi wa sehemu hiyo pamoja na kuongeza ajira. *(Makofi)*

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri ningependa kuuliza kwamba kwa kuwa mradi wa kuleta Gesi ya Songo Songo utakamilika mwezi Mei mwaka huu; je, kwa nini Serikali haikuwa na utaratibu wowote wa kuhakikisha ama Somanga Funga au *Mnazi Bay* inatoa umeme wa kutosha kwa ajili ya Mikoa ya Kusini?

Pili, kwa kuwa miradi ya umeme katika Mikoa ya Lindi na Mtwara yenye vyanzo vingi vya gesi, makaa ya mawe na *Stigler's Gorge* inalegalega mpaka sasa hivi; je, Wizara ya Nishati haioni kwamba haiwatendei haki watu wa Mikoa hii ya Kusini kwa kutokamilisha miradi ambayo itawahakikisha kwamba wanapata umeme wa kutosha katika maeneo haya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii nimhakikishie ndugu yangu Mheshimiwa Raynald Mrope kwamba Wizara ya Nishati na Madini hailegilegi katika kushughulikia masuala ya umeme kwa Mikoa ya Kusini na hususan kwa Mtwara na Lindi.

Kuhusu umeme ama wa Songo Songo au wa *Mnazi Bay,* nimeshawahi kutoa taarifa hapa Bungeni kwamba miradi hii yote miwili inafikiriwa kwa wakati mmoja. Lakini kutokana na gharama tofauti, ule mradi ambao utawahi na utaonekana kwamba una gharama nafuu ndio ambao utaanza kutekelezwa kwa soko la umeme la Mtwara na Lindi na pengine ningesema hapa kwamba kwa tathmini za awali, mradi wa kupeleka umeme kutoka *Mnazi Bay* unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 22, waakati ule wa kupeleka umeme kutoka Somanga Funga unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 36. Haya ndiyo mahesabu ya awali na kutokana na mahesabu haya ya awali, msisitizo mkubwa wa sasa hivi uko katika kupeleka umeme utakaotokana na gesi ya *Mnazi Bay* na hatua kubwa kabisa imefikiwa sio ya kutia saini ya awali yaani *Agreement of Intent* na Kampuni ya *Artumas Group Inc.* tu, lakini hatua kubwa imefikiwa ya sasa Kampuni hii kuwa katika hali ya kuweza kutafuta vyanzo makini vya fedha ya kutekeleza mradi huu. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wataalam husema kwamba chanzo kizuri cha uchumi mzuri ni matumizi ya kutosha ya maji, matumizi ya kutosha ya mawasiliano na uchukuzi na matumizi ya kutosha ya nguvu kwa maana ya umeme; na kwa kuwa karibu asilimia 20 ya maswali yanayoulizwa katika Bunge lako Tukufu yanahusu kupatikana kwa umeme kwa maendeleo ya Taifa letu; ni lini Serikali itaweka utaratibu wa kutosha ikapanga kuona kwamba umeme unapatikana ili kusudi maendeleo ya nchi hii yaweze kuinuka? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge juu ya umuhimu wa umeme kwa maendeleo ya nchi yetu.

Napenda pia nikubaliane naye juu ya wingi wa maswali ya umeme nchini. Lakini napenda niseme kwamba Serikali imefanya kazi kubwa ya usambazaji umeme nchini katika Makao Makuu ya Wilaya

mbalimbali na katika maeneo mbalimbali. Ndio maana tupo hapa tulipo hivi sasa kwamba tunaweza kuwa katika kiwango fulani cha maendeleo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali inao mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba maeneo mengi ya nchi yetu yana umeme wa uhakika. Hivi sasa utaratibu tayari umeandaliwa wa kuanzisha mfuko wa umeme Vijijini na Taasisi itakayoshughulikia usambazaji wa umeme Vijijini. Kwa taarifa tu, kabla ya Bunge hili Wizara imeshawahi kufanya Semina na Wajumbe wa Kamati ya Biashara na Uwekezaji juu ya Mfuko huu na tayari tulikuwa tumejiandaa kuja kuwafanyia Semina Waheshimiwa Wabunge kama tungekuwa tumepata nafasi ya kufanya Semina katika kipindi hiki cha Bunge. Upo utaratibu mahususi na nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba Serikali ina mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata nishati ya kutosha kwa maendeleo yetu. *(Makofi)*

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kuniona. Naomba nami niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa swali la msingi ni kusambaza umeme nchini, ili elimu iwe kamilifu *(comprehensive)* katika karne hii ya 21 ya sayansi na teknolojia, katika mazingira ya utandawazi, ili mwanafunzi aweze kupata elimu iliyo kamili kuanzia chekechea mpaka Chuo Kikuu lazima atumie *computer;* na kwa kuwa shule nyingi hapa nchini ziko Vijijini; je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba umeme unasambazwa huko Vijijini ili nao wanafunzi wapate elimu ya kutosha hasa katika maeneo ya Bukamba, Bulungwa kule Kahama? *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nilidhani ulishalijibu hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Raphael Mlolwa, juu ya umuhimu wa umeme katika kufundishia watoto wetu mashuleni kwa maana ya matumizi ya *Computer.*

Kama nilivyosema awali, Serikali imekuwa ikisambaza umeme Vijijini kupitia Shirika la *TANESCO.* Upo utaratibu huu ambao nimeutaja muda mfupi tu wakati najibu, lakini la ziada napenda niseme na nirejee hapa kwamba nimeshawahi kusema hapa Bungeni kwamba umeme sio umeme tu wa gridi ya Taifa unaosambazwa na *TANESCO* ambao unashughulikiwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, upo umeme pia wa *biogas* na nimewahi kusema hapa juu ya umuhimu wa kutumia umeme wa *biogas* hasa kwenye maeneo ya wafugaji kama ya ndugu zangu wa kisukuma kwamba katika maeneo haya kuna raslimali kubwa ambayo inaweza kutumika kwa ajili ya kutengenezea *biogas.*

Mheshimiwa Spika, upo Ushahidi kabisa katika maeneo mbalimbali katika Mikoa ya Tabora, Shinyanga na Mwanza ambapo katika baadhi ya Shule za Msingi kuna *biogas* inatumika katika kuendeshea shughuli za shule.

Ningependa nichukue nafasi hii nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwamba pale Wizarani kipo kitengo maalum kinachoshughulika na mambo ya *biogas* na tupo tayari kushirikiana naye kuhakikisha kwamba ile raslimali iliyopo Usukumani na Unyamwezi inaweza ikatumika vizuri katika kuzalisha *biogas. (Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Maswali kwa Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Mheshimiwa Henry Shekiffu.

Na.99

**Ujenzi wa Mabwawa kwenye Miinuko Wilayani Lushoto**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Lushoto ina miinuko *(undulating land)* inayowezesha ujenzi wa mabwawa kwa kuzuia vijito vidogo vidogo vinavyotoa maji kwa matumizi mbalimbali na kwa kuwa mpango wa

kuvuna maji kwa utaratibu wa kujenga mabwawa katika miinuko umeonesha mafanikio makubwa katika nchi zinazoendelea kama vile China na kadhalika na kwa kuwa mpango wa ujenzi huo wa mabwawa katika miinuko ulishaanza kutekelezwa Wilayani Lushoto miaka ya 1980 kwa madhumuni ya kilimo cha umwagiliaji na ufugaji wa samaki kama vile Bwawa la Kwabonda katika Kijiji cha Ngulwi ambao haukukamilishwa:-

(a) Je, Wilaya ya Lushoto iko katika mpango wa usambazaji maji kwa njia ya ujenzi wa mabwawa?

(b) Je, Serikali iko tayari kufanya uchunguzi zaidi na kuendeleza mabwawa yaliyokwishaanza kujengwa katika Jimbo la Lushoto kama lile la Kwabonda na Ngulwi?

(c) Kwa kuwa wananchi wa maeneo ya Kata ya Ngwelo na Mlola na Vijiji vya Kihitu Kigurunde, Ungo na Mazashi wamejitahidi sana kujenga mabwawa ya samaki; je, Serikali ipo tayari kuwasadidia wananchi hao kwa hali na mali (utaalam/mtaji) katika juhudi zao za kupambana na umaskini na kujiletea maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mbunge wa Lushoto, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Wilaya ya Lushoto inatekeleza mpango wa usambazaji maji kwa njia ya ujenzi wa mabwawa madogo madogo wa kushirikiana na Asasi isiyo ya Kiserikali ya Uimarishaji wa Kilimo cha Umwagiliaji wa Asili na Hifadhi ya Mazingira uitwao *(Traditional Irrigation and Environmental Development Organization - TIP).*

Kutokana na ushirikiano huo mabwawa madogo yenye uwezo wa kuhifadhi maji kati ya mita za ujazo 100 na 2,500 yanaendelea kujengwa kulingana na maombi kutoka kwa vikundi vya umwagiliaji vikionesha jinsi vilivyojiandaa. Mpango huo tangu uanze umewezesha kujenga mabwawa 15 yaani Tarafa ya Mtae mabwawa matano, Tarafa ya Soni mabwawa matano, Tarafa ya Mlalo mabwawa matatu, Tarafa ya Lushoto bwawa moja na Tarafa ya Mgwashi bwawa moja. Aidha, mwaka huu mabwawa mawili yanatarajiwa kujengwa katika Vijiji vya Soni na Sunga.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ipo tayari kufanya uchunguzi wa mabwawa katika Jimbo la Lushoto, kama vile katika maeneo ya Kwabonda na Ngulwi, mara pale uwezo wa kifedha utakaporuhusu.

Aidha, ninamshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee na juhudi zake za kuhamasisha wananchi kuchangia katika mradi unaoendelezwa na Asasi isiyo ya Kiserikali ili ujenzi wa mabwawa madogo ya Kwabonda na Ngulwi uweze kuendelea. Pia namshauri Mheshimiwa Mbunge aendelee na uhamasishaji wa wananchi kutunza mazingira ili kulinda vyanzo vya maji na upatikanaji wa maji safi na salama.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari wakati wowote kuwasaidia wananchi wa Kata za Ngwelo na Mlola pamoja na Vijiji vya Kihitu, Kigurunde, Ungo na Mazashi katika juhudi zao za kupambana na umaskini ili wajiletee maendeleo. Serikali ipo tayari kutoa ushauri wa kitaalam katika ujenzi wa mabwawa ya samaki mara itakapohitajika. Aidha, Serikali itatoa mchango wa fedha kulingana na uwezo wake unavyozidi kuongezeka.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, nina swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hawa wafadhili wa *TIP* wa Uholanzi walishaondoka na mabwawa yaliyojengwa ni machache sana, yako mabwawa ambayo yalianza kujengwa na Serikali hayajakamilika hasa bwawa la Kwabonda ambalo liko kijiji cha Ngulwi, je, Serikali inatamka nini kuhusu kulimalizia kulijenga bwawa hili ili litoe ajira kwa vijana na vile vile vijana waweze kufuga samaki?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli miradi mingi inayoletwa na wafadhili inatakiwa kuwa changamoto na kuchochea wananchi wenyewe na Halmashauri zetu ikiwemo Serikali kuingia katika kuendeleza miradi ambayo wananchi wanakuwa wameshaichagua.

Pia nakubaliana naye kwamba kuna mradi huo wa bwawa ambao haukumaliziwa lakini chini ya Mpango wa kutoa Huduma za Maji Safi na Mazingira katika Wilaya, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kupata taarifa na mradi huu kuwa tayari kupelekwa kwenye Wilaya ya Lushoto wakumbuke kuliingiza bwawa hilo katika ukarabati ili limaliziwe. Njia ambazo amezieleza zinazotumika China ni pamoja na uvunaji wa maji ya mvua ili kupunguza matatizo ya mahitaji ya maji katika vijiji vyetu.

Kwa hiyo, kwa wale wote ambao wana nyumba zilizoezekwa kwa mabati au vigae ni vema pia kuwahamasisha wananchi kama hao waweze kuvuna maji ya mvua ili kupunguza kutegemea maji ya kwenda kuchota kwenye visima au kwenye mabwawa. Nashukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kulitambua hilo na napenda akumbuke kuuingiza mradi huo baada ya mradi wa *World Bank* kupelekwa kwenye Wilaya ya Lushoto.

Na. 100

**Mradi wa Maji wa Nyakagomba - Chingunga**

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa maji ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu na kwa kuwa inaeleweka wazi kuwa maji ya visima katika Mkoa wa Mwanza si salama kutokana na kemikali za madini yaliyoko ardhini; ili kuokoa afya za wananchi wa maeneo hayo; je, Serikali ina mpango gani wa kufufua mradi wa maji wa Nyakagomba, Chankorongo Chikobe na Chigunga uliogharimu fedha nyingi sana bila kufanya kazi tangu mwaka 1976 na mabomba yanaozea chini ya ardhi?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mbunge wa Busanda, Wilaya yaGeita, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mradi wa maji wa Nyakagomba ulifanyiwa usanifu na kuanza kujengwa mwaka 1976. Kutokana na uhaba wa fedha mradi ulisimama kujengwa ilipofikia mwaka 1988 baada ya kutekeleza asilimia 85 tu ya matarajio ya mradi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002, mradi wa Nyakagomba ulifanyiwa tathmini kwa lengo la kuainisha mahitaji ya kukamilisha mradi huo kama ilivyotarajiwa. Baada ya kufanya tathmini hiyo ilionekana ni vyema mradi utekelezwe katika awamu mbili.

Awamu ya kwanza itakuwa ni kukamilisha ufungaji wa mabomba kwa vile hayakufungwa kwa ukamilifu katika baadhi ya sehemu ili maji yaweze kusambazwa na kutumiwa na wananchi. Awamu ya pili itakuwa ni kukamilisha sehemu ambazo mabomba hayakufungwa kabisa pamoja na ujenzi wa matanki na vituo vya kuchotea maji.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2002/2003 kiasi cha shilingi milioni 20 zilitengwa kwa ajili ya ukarabati wa awamu ya kwanza ya mradi. Fedha hizo zilitumika kununulia vipuli vya mashine ya kusukuma maji na kuitengeneza, kununulia mabomba, kuchimba mtaro na kufunga mabomba.

Katika kipindi cha mwaka 2003/2004 Wizara yangu imetenga kiasi cha shilingi milioni 10 kwa ajili ya kuendelea na ukarabati wa mradi huo. Kazi hii inatarajiwa kuendelea mara fedha zitakapotolewa.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kuanza kuufufua mradi huo lakini mradi huo

ulianza kujengwa mwaka 1976 wakati Wilaya ya Geita ilikuwa na wakazi kama 100,000 sasa hivi ina wakazi zaidi ya 700,000 karibu na Mkoa wa Lindi na inakaribia nchi ya Zanzibar, sasa Mheshimiwa Waziri pamoja na wataalam wanaweza kuja kuutembelea angalau kuona namna ya kuupanua kwa sababu Wilaya nzima ya Geita haina maji ili wananchi wa Geita ambao ni 700,000 waweze kupata maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ya Geita ina wananchi wengi ambao wanaingia karibu kila siku kutokana na shughuli zilizoko kule, shughuli za madini. Ni kweli pia kuwa mradi huo wakati unabuniwa mwaka 1976 ulitarajiwa kukidhi idadi ya wananchi wa wakati ule ambayo haikuwa kama ilivyo hivi sasa. Kwa kutambua hilo, Serikali imeiweka Wilaya ya Geita chini ya mradi wa Benki ya Dunia ambao utahudumia maji kwenye maeneo ya vijiji.

Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya kuhamasishwa na kuelekezwa kwa *Council* yake jinsi ya kutekeleza mradi huo ajaribu kukumbuka maeneo yote yenye shida ili kukidhi mahitaji ya maji safi na salama Wilayani Geita na kupunguza uwezekano wa Mheshimiwa Mbunge kulalamika kwamba maeneo yao mengi hayana miradi ya maji.

Na. 101

**Ongezeko Kubwa la Ujambazi**

**MHE. DAMAS P. NAKEI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika suala zima la utandawazi tumeshuhudia Serikali yetu ikijitoa katika shughuli za kibiashara na uchumi na kuziachia sekta binafsi; na kwa kuwa kazi ya Serikali sasa imebakia ni kusimamia ulinzi na usalama wa nchi pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Taifa:-

(a) Je, Serikali inatuambia nini kuhusu ongezeko kubwa na la kutisha la ujambazi nchini?

(b) Je, kwa nini tusiamini kwamba hali hiyo ya ujambazi kadri inavyoendelea, hatimaye itafikia hatua ya kuwa *Organized Crime* na kuvuruga amani ya nchi?

(c) Je, ni matukio mangapi ya ujambazi yametokea katika eneo la Mtungutu kwenye barabara itokayo Manyara - Dodoma tangu ulinzi uwekwe pale?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Damas Nakei, Mbunge wa Babati Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa vitendo vya ujambazi wa kutumia silaha nchini vimeongezeka katika miaka ya hivi karibuni ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Tatizo hili limejitokeza zaidi katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera na Kigoma. Hata hiyo, uhalifu huongezeka au hupungua kwa nyakati tofauti kutegemea na mambo mbalimbali ndani ya jamii nchini na hali ya usalama katika nchi jirani.

Kwa mfano, Mikoa ya mipakani Magharibi mwa nchi yetu ambayo huko nyuma haikuwa na matukio ya ujambazi wa kutumia silaha ilianza kuwa na matukio ya aina hiyo mwaka 1994 kufuatia wimbi la wakimbizi waliongia nchini kwetu baadhi wakiwa na silaha.

(b) Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Mbunge asiamini kwamba hali hiyo ya ujambazi inavyoendelea hatimaye itafikia hatua ya kujengeka mtandao wa magenge ya uhalifi *(Organized Crime)* na kuvuruga amani ya nchi kwa sababu Watanzania walio wengi wanachukia sana ujambazi na majambazi na wanatoa ushirikiano mkubwa kwa vyombo vya dola kuwafichua majambazi kwenye maeneo yao. Aidha, mikakati ambayo Serikali imeweka na kutekelezwa na Jeshi la Polisi kila mwaka haiwezi kutoa mwanya wa kuwepo *Organized Crime* kwa mfano.

(i) Wananchi wameanzisha vikundi vyao vya ulinzi wa jadi sehemu mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na Jimbo la Babati Magharibi na vikundi hivyo vinafanya kazi nzuri kudhibiti usalama katika maeneo yao wakisaidiana na vyombo vya dola.

(ii) Vile vile Jeshi la Polisi hufanya misako ya mara kwa mara katika maeneo yenye matukio mengi ya uhalifu kwa lengo la kuwatafuta na kuwakamata majambazi, kazi ambayo inaendelea kwa ufanisi wa kutosha.

(c) Mheshimiwa Spika, tangu Jeshi la Polisi liweke ulinzi katika eneo la Mtungutu kwenye barabara itokayo Babati - Dodoma jumla ya matukio saba ya ujambazi yametokea kama ifuatavyo:-

Mwaka 2000 matukio matatu, mwaka 2001 tukio moja, mwaka 2002 matukio mawili na mwaka 2003 tukio moja.

**MHE. DAMAS P. NAKEI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa matukio haya ya utekaji nyara, matukio ya ujambazi pia yanajitokeza katika Jimbo langu la Babati Magharibi, je, Serikali iko tayari kuweka kituo kidogo cha Polisi kwenye sehemu ya Mlima Dabii ambapo matukio haya yanatokea au Bashnet ili kudhibiti utekaji nyara ambao unazidi kuongezeka katika sehemu hiyo?

(b) Je, Serikali iko tayari kushirikisha Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili kusaidiana na Jeshi la Polisi katika kufanya operesheni maalum ya kutokomeza kabisa suala hili la ujambazi ambalo kwa kweli linasikika kila mara katika vyombo vyetu vya habari hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kukabiliana na ujambazi katika Jimbo lake, kwanza napenda kumuarifu kwamba baada ya Mkoa wa Manyara kukosa *RPC* kwa muda mrefu, juzi tumeshapeleka *RPC* katika Mkoa wa Manyara na yuko katika Jimbo lake. Kwa hiyo, naomba waitumie kwa ukamilifu ofisi mpya ya *RPC* kwa sababu ufagio mpya hufagia vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuweka kituo kidogo cha Polisi katika eneo alilolitaja la Mlima Dabii, Wizara yetu tuko tayari kushirikiana na wananchi kama wakianzisha mradi huo, tutakuwa tayari kwenda kuwaunga mkono lakini ni vizuri wananchi wenyewe waibue tatizo hilo waanze kutekeleza na sisi tutafika kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ametushauri kwamba kila inapowezekana tushirikishe Jeshi la Wananchi washirikiane na Jeshi la Polisi katika kufanya operesheni maalum. Huu utaratibu upo na mara kwa mara ndivyo tunavyofanya katika maeneo ambayo majambazi yamekithiri, huwa tunashirikisha vyombo vyote vya Dola vikisaidiana na Polisi kwenda kushughulikia tatizo hilo.

Mwaka jana tulifanya operesheni kama hiyo kule maeneo ya Kahama, Bukombe na tulifanya operesheni kubwa sana Mkoa wa Kagera Operesheni Kamaka na imekwenda vizuri sana. Kwa hiyo, utaratibu huu upo na tutaendelea kuutumia.

Na. 102

**Magari ya Zimamoto Mikoani na Wilayani**

**MHE. MARGARETH J. BWANA (k.n.y. MHE. MWANNE I. MCHEMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa majanga ya moto Mijini yanazidi kuongezeka siku hadi siku na magari ya Zimamoto hayapo na kama yapo ni mabovu kabisa na hayatumiki; na kwa kuwa Mikoa na Wilaya hapa nchini haina magari ya aina hiyo na hivyo moto unapotokea husababisha janga kubwa na hasara kwa mali za wananchi:-

(a) Je, ni Mikoa na Wilaya ngapi zenye magari ya Zimamoto na ni ipi haina na ni kwa sababu gani?

(b) Je, katika mwaka huu wa fedha 2003/2004 ni magari mangapi yanayotarajiwa kununuliwa na yatapelekwa kwenye Mikoa ipi?

(c) Je, ni lini Serikali ilinunua magari hayo kwa mara ya mwisho?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Mikoa yenye magari ya Zimamoto ni Dar es Salaam magari matatu , Mwanza gari moja, Dodoma magari matatu, Arusha magari matano, Morogoro magari mawili, Kilimanjaro magari mawili na Shinyanga magari mawili.

Kwa upande wa Wilaya, hakuna Wilaya yenye gari la Zimamoto lake yenyewe. Aidha, Serikali inayo magari ya Zimamoto kwa ajili ya vikosi maalum katika Viwanja vya Ndege na Bandari. Kikosi cha Zimamoto cha Viwanja vya Ndege kina jumla ya magari 18 ambayo yapo katika viwanja vya ndege vilivyoko katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Kigoma, Tabora, Kagera, Ruvuma *(Songea Airport),* Lindi *(Nachingwea* na *Lindi Airport),* Arusha, Dodoma na Mara *(Musoma Airport).*

Kikosi cha Bandari kina jumla ya magari 10 ambayo yapo katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara. Magari ya vikosi vya Viwanja vya Ndege na Bandari huitwa kusaidia kuzima moto unapotokea katika miji vilivyopo vikosi hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha yanatarajiwa kununuliwa jumla ya magari matano ya Zimamoto. Magari hayo yatasambazwa katika Manispaa za Kinondoni, Ilala, Temeke, Ilemela na Nyamagana.

(c) Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho kwa Serikali kununua magari ya Zimamoto ni mwaka wa fedha uliopita 2002/2003 ambapo shilingi bilioni 1.5/= zilitumika kununua magari mawili kwa ajili ya kuimarisha Kikosi cha Zimamoto cha Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa jumla kujielimisha kuhusu namna ya kuepuka majanga ya moto na pia namna ya kutumia zana ndogo ndogo za kuzimia moto *(portable fire extinguishers).*

**MHE. MARGARETH J. BWANA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa Mikoa na Wilaya nyingi hapa nchini hazina magari ya Zimamoto, je, Serikali itakuwa tayari kuwaondolea kodi wafanyabiashara wenye uwezo wa kununua magari haya ili yaweze kusambazwa Mikoani na Wilayani katika kusaidia janga hili la moto pindi unapotokea?

(b) Kwa kuwa Kiwanda cha Nyumbu kina uwezo mkubwa wa kutengeneza magari ya Zimamoto na wamewahi kutengeneza magari haya wakishirikiana na kampuni moja ya Ireland na magari haya yakauzwa hadi Marekani, je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kukisaidia kiwanda hiki ili kukiongezea nguvu ili kiweze kutengeneza magari haya na kuyasambaza katika maeneo mbalimbali yenye upungufu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba maeneo mengi hayana magari ya Zimamoto na ni kweli kuwa magari ya Zimamoto bei yake ni kubwa sana ndio maana wengi wanashindwa kuyanunua, pendekezo lake kwamba Serikali itazame uwezekano wa kuondoa kodi na ushuru ni pendekezo zuri tutalifikisha katika Wizara ya Fedha ili liweze kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kutumia kiwanda cha Nyumbu kutengeneza magari ya Zimamoto, kwanza ni kweli kwamba Shirika la Nyumbu ambalo liko chini ya Jeshi la Wananchi linao uwezo huo na ilikwishaanza kuutumia, bahati mbaya hapa katikati likakumbwa na matatizo kwa hiyo halikuendelea tena kutengeneza magari mengine lakini katika *budget speech* ya Waziri wa Ulinzi na JKT katika mashirika ambayo alisema kwamba sasa Serikali inayafufua kwa kuyawezesha ni pamoja na Shirika la Nyumbu. Kwa hiyo, vile vile ni wazo zuri Waziri wa Ulinzi yuko hapa ahadi ipo kwa hiyo Shirika hili tutaliimarisha ili litekeleze jukumu hili.

Na. 103

**TBS Kutoa Ubora wa Maji ya Bomba**

**MHE. DR. MWITA HAJI MWITA (k.n.y. MHE. ISSA MOHAMMED SULEIMAN)** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Tanzania wanakiamini chombo cha *TBS* kwa kujua kuwa chombo hicho kinawahakikishia ubora wa bidhaa wanazozitumia kama vile maji ya chupa tunayokunywa na kadhalika:-

(a) Kwa kuwa *TBS* iko kimya juu ya ubora na usalama wa maji ya bomba ambayo Watanzania wengi huyatumia, je, ndiyo kusema kwamba maji hayo sio safi?

(b) Kwa kuwa *TBS* haijatoa taarifa ya aina hiyo hata kwa Mkoa wa Dar es Salaam, je, hakuna umuhimu wa Watanzania kupewa taarifa hiyo?

(c) Je, ni lini *TBS* itawaondolea wananchi wasiwasi juu ya ubora na usafi wa maji ya bomba kwa Tanzania nzima ili maji hayo yatumiwe kwa raha?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Mohamed Suleiman, Mbunge wa Magomeni, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Shirika letu la Viwango Tanzania yaani *TBS,* kwa kutambua majukumu yake limekuwa likishauriana na Wizara inayohusika na Maji kuhusu viwango vya maji, yakiwemo maji ya bomba kwa ajili ya kuhakikisha usafi na usalama wa maji hayo kwa watumiaji. Kutokana na mawasiliano hayo, Kamati ya wataalam imeundwa chini ya Mwenyekiti mtaalam toka Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kwa ajili ya kuandaa viwango vya maji ya bomba. Tayari kwa sasa rasimu ya awali ya kiwango cha maji ya bomba imeandaliwa na hatua kadhaa zinahitajika kabla kiwango hicho hakijapewa hadhi ya kiwango cha Kitaifa.

Hatua hizo ni pamoja na kuhakikisha wadau wanafahamishwa kuhusu kiwango ili wapate nafasi ya kutoa maoni yao kitaalam ambayo yakikubalika yanatengeneza kiwango. *TBS* itatoa taarifa rasmi baada ya kukamilisha hatua hizo. Hata hivyo inasisitizwa kuwa wananchi wa Dar es Salaam na Mikoa mingine waendelee na tabia ya kuchemsha maji ya bomba ambayo wanatumia kunywa kwa vile mabomba mengi ya Dar es Salaam ni machakavu na kuna uwezekano mkubwa wa maji hayo, ingawaje meupe, kubeba vijidudu pale yanapopita mahali ambapo bomba limepasuka.

(b) Mheshimiwa Spika, *TBS* haijatoa taarifa yoyote kwa vile hatua za kukamilishwa kiwango hicho haijakamilika. *TBS* itatoa taarifa kuhusu kiwango cha maji ya bomba mara tu baada ya kukamilisha zoezi la kuweka kiwango hicho.

(c) Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa kiwango cha maji ya bomba ni jambo moja lakini utumiaji wa kiwango hicho ili kuhakikisha kuwa maji ni safi na salama ni jambo lingine. Kama inavyofahamika zipo Mamlaka katika kila miji zinazosimamia upatikanaji wa ugavi wa maji ya bomba. Hivyo baada ya

kiwango kuwepo itakuwa ni jukumu la Mamlaka zote hizo kuzingatia kiwango hicho ili maji ya bomba yawe safi na salama. *TBS* itatoa kiwango kwa ajili ya mamlaka hizo kutumia na kutoa maji safi. Kwa sasa tunaomba wananchi waendelee na tabia njema ya kuchemsha maji ya kunywa.

**MHE. DR. MWITA HAJI MWITA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa hivi sasa kumekuwa na mtindo hasa katika Jiji la Dar es Salaam vijana kuuza maji ya *packet* kwenye ndoo, je, Mheshimiwa Waziri anatuhakikishia nini kuhusu usalama wa maji haya ambayo sasa hivi yameenea sana?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba vijana wengi Dar es Salaam wanauza maji na Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Manispaa zake wamewatahadharisha wananchi kuwa wasiamini sana yale maji na imedhihirika wazi kuna wakati wanachota maji machafu, wanachimba maji yenye chumvi na hayajawekwa aina yoyote ya dawa kwa sababu maji ya bomba kubwa yanayotoka Ruvu yanawekwa asilimia zinazohitajika kwa ajili ya kuuwa vijidudu katika maji yale. Kwa hiyo, hatuwezi kabisa kuwahakikishia wananchi kwamba yale maji ni salama bado tunasisitiza kwamba wachemshe maji.

Na. 104

**Udhibiti wa Bidhaa Zinazoingizwa Nchini Kimagendo**

**MHE. JACOB D. SHIBILITI** aliuliza:-

Kwa kuwa baada ya ubinafsishaji wa baadhi ya viwanda vyetu kama vile Kampuni ya Bia, Sigara na mashirika mengine nchini, uzalishaji umeongezeka:-

(a) Je, Serikali inawalindaje wazalishaji hao dhidi ya bidhaa zinazoingizwa nchini kwa njia ya magendo kwa kutumia nembo za kampuni zinazomiliki bidhaa hizo?

(b) Kwa kuwa Kampuni ya Sigara ina wasiwasi juu ya Sigara bandia zinazohisiwa kutoka nchi jirani kwa kutumia nembo hiyo; je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo na itasaidia vipi kukomesha hali hiyo ambayo inaathiri kwa kiwango kikubwa ubora wa bidhaa halisi na soko kwa kampuni husika?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mbunge wa Misungwi, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali imetunga Sheria ya Alama za Biashara na Huduma ambayo ikitumiwa vizuri tatizo hili litakomeshwa. Chini ya Sheria hii mtu haruhusiwi kutumia alama ya mtu mwingine bila idhini yake. Kama ikitokea mtu huyo kutumia alama ya mwenzake bila idhini, mmiliki wa alama hiyo anao uwezo wa kumfungulia mashtaka na kudai fidia kwa kitendo hicho. Hili limeainishwa chini ya kifungu Na.32 cha Sheria ya Alama za Biashara na Huduma ya mwaka 1986.

Aidha, chini ya Sheria hii Kifungu Na.59 kinatoa mwanya wa kufungua mashtaka ya jinai dhidi ya mtu yeyote anayekiuka sheria hii ambapo adhabu yake ni faini au kifungo kisichozidi miaka mitatu au vyote viwili.

(c) Kampuni ya Sigara ina haki ya kutumia Sheria ya Alama za Biashara kwa kuwafungulia mashtaka wote wale wanaoagiza sigara toka nje ambazo zinatumia nembo ya kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali inakemea vikali wafanyabiashara ambao wanatumia hila mbalimbali kuingiza bidhaa nchini kwa magendo, kukwepa kulipa ushuru sahihi na kutumia nembo ambazo sio za kwao.

Hali hii inaleta ushindani usio wa haki kwa viwanda vyetu. Vyombo mbalimbali vya Serikali inabidi vishirikishwe kudhibiti hali hii inayozorotesha ufanisi wa viwanda vyetu na kuathiri ajira. Vinginevyo nchi yetu itageuzwa kuwa dampo la bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya wengine hata pale ambapo wawekezaji wamejenga viwanda vya aina hiyo hapa nchini.

Katika misingi hii tumepitisha sheria ya kuzuia uingizaji holela wa bidhaa *(Anti- Dumping)* na Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa lengo la kudhibiti ushindani usio wa haki kwa viwanda vyetu unaotokana na ukwepaji kodi, uingizaji bidhaa hafifu na matumizi bandia ya alama za biashara. Wizara iko tayari kupokea malalamiko rasmi kutoka viwanda vinavyoathiriwa na hali hii.

**SPIKA:** Huo ndio mwisho wa maswali kwa siku ya leo na muda wa maswali vile vile umekwisha.

Kabla hatujaendelea, kama kawaida kuna matangazo ya vikao vya Kamati kwa siku ya leo navyo ni kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni Kamati ya Ulinzi na Usalama, Mwenyekiti wake anaomba Wajumbe wakutane leo tarehe 11 Februari, 2004, saa tano asubuhi, ukumbi namba 133 katika kumbi za Kamati, ghorofa ya kwanza.

Pili, Kamati ya Miundombinu, Mwenyekiti anaomba niwatangazie Wajumbe wake kwamba wakutane leo tarehe 11 Februari, 2004, saa tano asubuhi, ukumbi namba 219, *Wing B,* ghorofa ya pili.

Kamati ya tatu na ya nne, kuna Kamati mbili Wenyeviti wao wamepanga zikutane kwa pamoja nazo ni Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Kamati ya Huduma za Jamii, wamepangiwa kukutana saa saba mchana na madhumuni ya kukutana ni kuonana na kubadilishana mawazo na watu wenye ulemavu. Waliomba hivyo na wamekubaliwa kukutana na Kamati zote mbili saa saba mchana.

Tano, Kamati ya Mheshimiwa Dr. William Shija, Kamati ya Mambo ya Nje nayo, anaomba Wajumbe wake wakutane saa tano asubuhi hii, ukumbi namba 231, ghorofa ya pili kwa madhumuni ya kuonana na Mheshimiwa Balozi wa Korea ya Kusini pamoja na Balozi wa Uingereza.

Pia Mheshimiwa William Shellukindo, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hiyo kuwa kutakuwa na kikao cha Kamati leo tarehe 11 Februari, 2003 mara baada ya kipindi cha maswali na majibu, chumba namba 428, ghorofa ya nne. Ndiyo hizo Kamati ambazo Wenyeviti wake wamepanga zikutane leo.

Sasa la pili, linahusu ratiba ya kesho. Waheshimiwa Wabunge tumeshawagawia ratiba ya ujio wa Mheshimiwa Rais kesho na mtaona kwenye ratiba hiyo kwamba kuna mambo mengine ya itifaki ambayo huwa tunayafanya kwa kawaida Mheshimiwa Rais anapokuja, lakini hatutayafanya kesho. Hii ni kwa sababu ya maradhi ya mguu aliyonayo,kwa hiyo tusingependa apande pande ngazi na kukagua kagua magwaride.

Kwa hiyo, hayo mambo mengine ambayo tumezoea kuyaona hayatakuwepo. Lakini kama ratiba inavyoonyesha hakutakuwa na kipindi cha maswali, kwa hiyo, kama mnavyofahamu Waheshimiwa Wabunge kila siku ya kikao inapangiwa maswali yake, wauliza maswali wanajulishwa na Mawaziri wanaojibu vile vile.

Kwa hiyo, ni vigumu kuvuruga ratiba hiyo na tulipoipanga tulikuwa hatujajua kwamba Mheshimiwa Rais atakuja kulihutubia Bunge. Kwa hiyo, tulichokubaliana kufanya ni kuyahamisha maswali ya kesho yote yapangiwe siku nyingine, siyo kuyasogeza mbele, yapangiwe siku nyingine labda mwishoni mwa Mkutano huu ili tusivuruge ratiba ambayo imekwishapangwa.

Nafikiri ndiyo hayo matangazo ya leo. Nieleze tu vile vile kwamba Rais mwenyewe alitaka tuwaalike Wenyeviti wote wa Vyama vya Siasa ambavyo vina usajili wa kudumu. Tumefanya hivyo na

Wenyeviti kumi na moja wameshathibitisha kwamba watakuja, mpaka tulipofunga kazi jana jioni, Vyama 11 vilishathibitisha kwamba vitahudhuria. Kwa hiyo, nadhani tutakuwa na *full House.*

Kwa ajili ya ujio wa Mheshimiwa Rais kesho tumemwalika vile vile Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, naye amekubali kuhudhuria, lakini kwa mila na desturi za Bunge mtu asiyekuwa Mbunge hawezi kuingia katika ukumbi huu bila idhini ya Bunge lenyewe. Kwa hiyo, sasa nitamwomba *Chief Whip* wa Serikali atoe hoja ya kuomba idhini hiyo ili Bunge limruhusu Mheshimiwa Makamu wa Rais aweze kuingia hapa kesho. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**HOJA YA KUMRUHUSU MAKAMU WA RAIS KUHUDHURIA HOTUBA YA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA BUNGENI DODOMA TAREHE 12 FEBRUARI, 2004**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, naomba ruhusa ya Bunge lako Tukufu likubali Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aingie ndani ya ukumbi huu kesho tarehe 12Februari, 2004.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Hoja ya kumruhusu Makamu wa Rais kuhudhuria hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Bungeni Dodoma Tarehe 12 Februari, 2004 ilikubaliwa na Bunge)*

**HOJA ZA SERIKALI**

**MAAZIMIO**

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia*(The Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty (CTBT)***

**Azimio la Kuridhia Mkataba Kuruhusu Ufunguzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kupima na Kufuatilia viwango vya Mionzi Ayonisha katika Mazingira Chini ya Tume ya Kimataifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty Organization (CTBTO)***

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo kuhusu Azimio au Maazimio husika napenda kuchukua nafasi hii kuwatakia kheri ya mwaka mpya wa 2004 wewe mwenyewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote. *(Makofi)*

Aidha, naomba pia niwapongeze Waheshimiwa Getrude Mongella, Athuman Janguo, Remidius Kissassi, Dr. William Shija na Dr. Amani Walid Kabourou, kwa kuchaguliwa kwao na Bunge hili kutuwakilisha katika Bunge la Afrika.

Pia naomba kumpongeza Mheshimiwa Sophia Simba, kwa kuchaguliwa kutuwakilisha katika Bunge la *SADC.* Napenda pia kuzielekeza pongezi zangu kwa Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge wa Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, historia ya Mkataba wa Kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(CTBT)* inaanzia mwaka 1968 wakati Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa *(The General Conference or General*

*Assembly)* lilipopitisha Mkataba wa kupiga vita uendelezaji wa matumizi ya silaha za nyuklia *(The Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty (NPT)).* Hatua hii ilichukuliwa baada ya madhara makubwa ya matumizi ya silaha za nyuklia kuonekana wakati wa vita vya pili vya dunia huko Japan katika Miji ya Hiroshima na Nagasaki. Katika miaka ya karibuni baadhi ya nchi zimekuwa zikitishia kutumia silaha za nyuklia katika vita na hivyo kutishia amani ya dunia. Hivyo basi jumuiya ya Kimataifa imeamua kuchukua hatua thabiti ili kuhakikisha kwamba silaha hizo hazitengenezwi wala kutumiwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitishwa kwa *The Non Proliferation Treaty (NPT)* nchi nyingi duniani zikiwemo za dunia ya tatu zilisaini na kuridhia Mkataba huo. Tanzania ilikubali Mkataba huo katika miaka ya 90 ingawa bado haijauridhia. Vile vile Tanzania ni mwanachama yaani imeweka sahihi wa Mkataba mwingine uitwao *The Africa Nuclear Free Zone Treaty* ambao unajulikana vile vile kama *The Perindaba Treaty.* Mikataba yote hiyo na harakati zote hizi za Kimataifa zinalenga kuiepusha dunia na matumizi ya silaha za nyuklia ambazo zina madhara makubwa kwa binadamu na mazingira yake.

Mheshimiwa Spika, katika harakati za aina hiyo Mkataba wa Kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(CTBT)* ulipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 10 Septemba, 1996 kwa Azimio Na. 50/245 na ukafunguliwa kwa ajili ya kutiwa saini na Mataifa yote tarehe 24 Novemba,1996. Hadi kufikia mwaka 2003 nchi nyingi zikiwemo za Afrika zimetia saini na kuridhia Mkataba huo. Tanzania bado haijasaini wala kuridhia Mkataba wenyewe. Kwa faida ya Bunge lako Tukufu, nchi za Kiafrika zilizokwisharidhia Mkataba huu ni Algeria, Botswana, Eritrea, Gabon, Kenya, Lesotho, Libya, Mali, Mauritania, Morocco, Namibia, Niger, Nigeria, Senegal, Sierra Leone, *South Africa* na Uganda.

Mheshimiwa Spika, zipo hatua mbalimbali za kufuatwa katika utekelezaji wa Mkataba huu. Mojawapo ni kuundwa chombo kitakachosimamia utekelezaji wa Mkataba ambacho ni *The Comprehensive Test Ban Treaty Organization (CTBTO)* ambapo kila nchi iliyotia saini Mkataba huo itakuwa mwanachama na pia kuanzishwa kwa Mtandao wa Kufuatilia Milipuko ya Nyuklia *(International Monitoring System (IMS).* Katika mtandao huo kutaanzishwa vituo vya aina nne:-

(a) *Radio Nuclide Monitoring Stations;*

(b) *Cesium Logical Monitoring Stations;*

(c) *Hydraquistic Monitoring Stations; and*

(d) *Infrasound Monitoring Stations.*

Mheshimiwa Spika, vituo hivyo vitaanzishwa katika nchi mbalimbali kulingana na *survey* ya kitaalam iliyofanyika na bila kujali kama nchi itakayohusika na kituo hicho ni mwanachama au *part* wa *CTBT* au la. Tanzania imechaguliwa kuwa mwenyeji wa kituo kimojawapo cha *Radio Nuclide Monitoring* ambacho kimependekezwa kujengwa Dar es Salaam kutokana na sababu za kijiografia.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya nchi wanachama wa *CTBT (basic obligations),* yameelezwa katika Ibara ya (1) ya Mkataba huu ambayo ni kama yafuatayo:-

(a) Kila nchi mwanachama haitakiwi kufanya majaribio yoyote ya silaha za nyuklia au nguvu za nyuklia.

(b) Kupiga marufuku na kuzuia milipuko ya kinyuklia mahali popote kwenye himaya yake.

(c) Kila nchi mwanachama anatakiwa kuachana na kusababisha au kutia moyo au kwa njia yoyote ile kushiriki katika majaribio ya silaha ya nyuklia.

(d) Kila nchi mwanachama atakuwa na wajibu wa kushirikiana na *CTBT* ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kulingana na Mkataba wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa kuridhia *CTBT.* Nchi inayotaka kuridhia Mkataba wa *CTBT* haina budi kufuata utaratibu iliojiwekea yenyewe kikatiba. Kwa nchi kama Tanzania utaratibu wa kuridhia Mikataba ya Kimataifa hauna budi ufuatwe ambapo Serikali kupitia Wizara husika inatakiwa ipeleke hoja Bungeni ili Bunge liweze kutoa tamko au azimio la kuridhia *(ratification declaration)* na hivyo kuufanya Mkataba huo kuwa sehemu ya sheria za nchi.

Baada ya Bunge kutoa tamko au Azimio hilo, tamko au azimio hilo litawekwa kisheria, *ratification instrument* itatengenezwa na baadaye kupelekwa kwa mhifadhi anayeitwa *depository* wa nyaraka hizo ambaye kwa mujibu wa *CTBT* ni Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa.

Mheshimiwa Spika, gharama za kuridhia *CTBT.* Nchi inayoridhia Mkataba huu na hivyo kuwa mwanachama wa *CTBTO* itawajibika kuchangia kiasi cha fedha za Kitanzania milioni tano na nusu kwa mwaka kwa ajili ya kuendesha na kutekeleza Mkataba huo chini ya *CTBTO.* Tanzania inatarajia kutozwa kiasi kidogo cha mchango huo kulingana na uwezo wake mdogo wa kifedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu faida za kuridhia Mkataba huu. Faida za kuridhia Mkataba huu zipo nyingi lakini sababu kubwa ni kwamba Tanzania tayari imekwishachaguliwa kuwa moja ya nchi wenyeji wa kituo cha *Radio Nuclide Monitory* kama ilivyoelezwa kwenye utangulizi. Hivyo basi Tanzania kama mwanachama wa *CTBTO* itanufaika na taarifa zinazopatikana katika kituo hicho na hata vituo vingine kupitia kile kinachoitwa *International Data Centre* kituo kilichopo Vienna, Austria kwa ajili ya masuala ya utafiti na elimu, ulinzi na usalama na kuwa sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa katika kudhibiti matumizi yasiyo ya amani na salama ya nguvu za atomiki.

Aidha, Tanzania kama mwanachama wa *CTBTO* itaendelea kupokea misaada ya kiufundi inayohusu nguvu za atomiki na teknolojia ya nyuklia ambayo hutolewa kupitia Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani *(The Internation Atomic Energy Agency)* lenye Makao Makuu yake huko Vienna, Austria. Pia Tanzania itapata fursa ya kuwa na sauti sawa kwenye maamuzi yote yanayohusu matumizi ya nguvu za nyuklia kama ilivyoelezwa katika Mkataba huu wa *CTBT* na kushiriki shughuli zote za *CTBTO.*

Mheshimiwa Spika, haitarajiwi kuwepo kwa athari zozote kwa Tanzania kwa kuridhia Mkataba huu hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania haitarajiwi kuwa na programu za kutengeneza silaha za nyuklia. Mpaka sasa ni nchi 170 zimeshatia saini Mkataba huu na nchi 109 zimekuwa katika *monitoring system* ambazo unasimamia kuhakikisha nchi zinafuata na kutimiza masharti ya Mkataba huu ambao unahusu uzuiaji, ulipuaji na majaribio ya nyuklia. Mtandao huu una vituo 321 na maabara 16 za teknolojia ya *Radio Nuclide* ambao kazi yake kubwa ni kuhakiki na kudhibiti milipuko ya nyuklia.

Kama mlipuko wa nyuklia ukitokea mambo mawili makubwa huambatana nayo ni kwanza nishati ya nyuklia inajitokeza. Pili, chembechembe za vyanzo vya mionzi hutoka ambazo hushikana na nishati hiyo kwenye mazingira na kusambaa kama mawimbi ya sauti kwenye ardhi, baharini na kwenye hewa. Mtandao wa teknolojia utakaotumika nchini Tanzania ni wa aina ya *Radio Nuclide,* mtandao huu una vituo 80 na unatambua chembechembe za vyanzo vya mionzi kwenye hewa, ardhini na majini ikiwa mlipuko wa nyuklia utatokea.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi, sasa naomba kusoma maazimio yenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Tanzania ni moja ya nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa;

NA KWA KUWA nchi zote duniani zinakabiliwa na matatizo ya matumizi yasiyo salama wala ya amani ya nishati ya nyuklia na utengenezaji wa silaha za nyuklia;

NA KWA KUWA Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test Ban (CTBT)* mwaka 1996;

NA KWA KUWA kupitishwa kwa Mkataba huu ni sehemu ya juhudi za Kimataifa za kupiga vita utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia chini ya Mkataba wa *The Non Proliferation of Nuclear Weapons Treaty (NPT);*

NA KWA KUWA sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 imeelekeza matumizi salama na ya amani ya nishati ya nyuklia katika sekta mbalimbali za maendeleo kama vile afya, elimu, kilimo na nishati pamoja na udhibiti wa mionzi ayonisha inaweza kuzagaa katika mazingira yetu;

NA KWA KUWA Tanzania ilikubali Mkataba huu lakini bado haijauridhia na ambapo Tanzania ni mwanachama wa Mkataba mwingine uitwao *The African Nuclear Free Zone Treaty (The Perindaba Treaty);*

NA KWA KUWA kulingana na Mkataba wa *CTBT* kunahitajika kuanzishwa kwa mitandao ya kupima na kufuatilia viwango vya mionzi ayonisha katika mazingira;

NA KWA KUWA katika mtandao huo vituo vya aina nne vinatakiwa kuanzishwa katika nchi mbalimbali duniani ambavyo ni udhibiti wa mionzi katika mazingira, udhibiti wa matetemeko ya ardhi, udhibiti wa mawimbi ya maji na udhibiti wa mawimbi ya sauti ya ardhini;

NA KWA KUWA faida za kuridhia Mkataba huu ni nyingi ambazo ni pamoja na Tanzania kuweza kushiriki shughuli zote za *CTBT* na kuendelea kupokea misaada ya kiufundi inayohusu maendeleo na matumizi ya teknolojia ya nyuklia kupitia Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani. Pia kupata taarifa zitakazopatikana kwa ajili ya masuala ya utafiti, mazingira, elimu, ulinzi na usalama katika kituo hicho na hata mtandao wa vituo vingine duniani kupitia *International Data Centre* kilichopo Vienna, Austria;

KWA HIYO BASI, kwa kutambua umuhimu wa kuridhia Mkataba huu wa Kimataifa kwa mujibu wa Ibara ya 63(3e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Bunge hili katika Mkutano wake wa 14 sasa linaazimia Tanzania kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty).*

Mheshimiwa Spika, naomba nisome na Azimio ambalo linaambatana na hili yaani Azimio la Itifaki ya Kimataifa ya Kuruhusu Ufunguzi wa Kituo cha Mataifa cha Kupima na Kufuatilia Mionzi Ayonisha katika Mazingira Chini ya Tume ya Kimataifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty Organization)*

KWA KUWA Tanzania ni moja ya nchi mwananchama wa Umoja wa Mataifa;

NA KWA KUWA Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha Mkataba wa Kimataifa wa kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty)* kwa Azimio Na. 50124;

NA KWA KUWA kupitishwa kwa Mkataba huu ni sehemu ya juhudi za Kimataifa za kupiga vita utengenezaji na matumizi ya silaha za nyuklia kama sehemu ya utekelezaji wa Mkataba wa amani wa *The Non Proliferation of Nuclear Weapon Treaty;*

NA KWA KUWA chini ya Mkataba huo kiliundwa chombo cha kusimamia utekelezaji wake ambacho ni Tume ya Kimataifa ya huu udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty Organization CTBTO);*

NA KWA KUWA kulingana na Mkataba wa *CTBT* kunahitajika kuanzishwa kwa mitandao ya kupima na kufuatilia viwango vya mionzi ayonisha katika sehemu mbalimbali;

NA KWA KUWA sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia inaelekeza matumizi salama na ya amani ya nguvu za nyuklia katika sekta za afya, nishati na sayansi pamoja na udhibiti wa mionzi ayonisha inayoweza kuzagaa katika mazingira yetu;

NA KWA KUWA Tanzania imeombwa kufungua Kituo cha Kimataifa cha Kupima na Kufuatilia Viwango vya Mionzi Ayonisha *(Radio Nuclide Monitoring Station (RMSD)* katika mazingira nchini na kuendeshwa na Tume ya Maandalizi ya Mkataba wa Kimataifa kuhusu Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia;

NA KWA KUWA kituo kitakachofunguliwa Tanzania kitakuwa ni kimojawapo cha mtandao wa vituo 80 vinavyotarajiwa kuanzishwa na kuendeshwa chini ya Mkataba huo kama ilivyopangwa kulingana na nafasi zao za kijiografia katika nchi mbalimbali duniani;

NA KWA KUWA mtandao huo umebuniwa kitaalam ili kukidhi uwezekano wa upatikanaji wa taarifa za majaribio ya silaha za nyuklia au milipuko asilia na ile isiyo asilia au uchafuzi wa aina yoyote unaotokana na vyanzo vya mionzi katika mazingira;

NA KWA KUWA mtandao wa Kimataifa wa kudhibiti mionzi ayonisha ni mmoja katika mitandao minne inayotarajiwa kufunguliwa kama sehemu ya udhibiti wa Kimataifa *(International Monitoring System (IMS)* chini ya Mkataba huu ambao ni udhibiti wa mionzi katika mazingira, udhibiti wa matetemeko ya ardhi, udhibiti wa mawimbi ya maji na udhibiti wa mawimbi ya sauti ya ardhini;

NA KWA KUWA kituo kitagharamiwa na kuendeshwa na *CTBTO* kwa kushirikiana na chombo kinachosimamia masuala ya mionzi na nguvu za atomiki nchini;

NA KWA KUWA Serikali itabidi itoe jengo la kusimika vifaa vya uchunguzi, wataalam wa kizalendo katika fani ya mionzi na kutenga kiasi cha shilingi milioni moja katika Bajeti ya Wizara kwa ajili ya uendeshaji wa kituo;

NA KWA KUWA ufunguzi wa kituo utatoa nafasi nzuri ya kufanya utafiti kuhusu nguvu za atomiki, kupata taarifa kuhusu milipuko ya kinyuklia na kuweza kujiandaa jinsi ya kukabiliana nayo, kushirikiana na jumuiya ya Kimataifa katika udhibiti wa matumizi yasiyo salama na ya amani ya nguvu za nyuklia;

NA KWA KUWA kutofanikisha ufunguzi wa kituo hiki cha Kimataifa kutaathiri kwa kiwango kikubwa utendaji wa Tume ya Kimataifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia;

KWA HIYO BASI, kwa kuzingatia umuhimu wa kuridhia itifaki hii ya Kimataifa na kwa mujibu wa Ibara ya 63(3e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, Bunge hili katika mkutano wake wa 14 sasa linaazimia Tanzania kuridhia Itifaki ya Kimataifa ya kuruhusu ufunguzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kupima na Kufuatilia Viwango vya Mionzi Ayonisha katika Mazingira chini ya Tume ya Kimataifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The International Monitoring System under the Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty Organization).*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wajumbe, hoja mbili zimetolewa kwa pamoja na zitajadiliwa kwa pamoja. Ningependa kueleza vile vile kwa ajili ya ujio wa kesho, tungependa ikiwezekana kikao cha leo kiishe mapema ili tuache ukumbi uwekwe katika hali ya kupokea ugeni wa kesho na inaelekea hilo litawezekana kwa sababu kwa kulingana na maombi niliyonayo nina ombi moja tu kwa Azimio la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia. Sina ombi kwa kuchangia hoja inayofuata na nina ombi moja tu kuhusu Muswada uliopo kwenye *Order Paper.* Sasa kama hivyo ndivyo tunaweza tukamaliza saa saba ili kusudi kipindi cha mchana tukiache wazi. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati yenye *portfolio* ya Wizara hii atoe maelezo ya Kamati kuhusu Mikataba yote miwili.

**MHE. OMAR S. KWAANGW' - MWENYEKITI WA KAMATI YA HUDUMA ZA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Huduma za Jamii kuhusu Azimio la Bunge la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty CTBT)* pamoja na Itifaki ya Kimataifa ya Kuruhusu Ufunguzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kupima na Kufuatilia Mionzi Ayonisha katika Mazingira chini ya Tume ya Kimataifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test Ban Treaty Organization (CTBTO).*

Mheshimiwa Spika, maoni ya kuridhia Mkataba na Itifaki nayatoa kwa pamoja. Kwanza kwa niaba ya Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii naomba nichukue nafasi hii kuwapa kheri Waheshimiwa Wabunge kwa mwaka wa 2004.

Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuungana na sisi katika Bunge hili. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kutuwakilisha kwenye Bunge la Afrika. Vile vile Mheshimiwa Sophia Simba, kuwa mwakilishi wetu kwenye *SADC Parlimentary Forum. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilifikiria maazimio ya Bunge ya kuridhia Mkataba wa Itifaki ya Kimataifa niliyoitaja hapo juu. Kamati ilipitia maelezo na ufafanuzi toka kwa Mheshimiwa Waziri wa Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu akisaidiwa na Naibu wake pamoja na wataalam.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikubaliana na maelezo yaliyotolewa kuwa nchi zote duniani zinakabiliwa na matatizo ya matumizi yasiyo salama wala ya amani ya nishati ya nyuklia na utengenezaji wa silaha za nyuklia. Kamati iliridhika na kuunga mkono hatua ya Serikali ya kuleta maazimio ya kuridhia Mkataba na Itifaki ya Kimataifa ya kukabiliana na tishio la matumizi mabaya ya nishati ya nyuklia ili yaridhiwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hatua ya Serikali kuleta maazimio haya ili yaridhiwe na Bunge Kamati ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua yake ya kutaka kuridhia Mkataba wa Kimataifa na Itifaki ya Kimataifa ya Kudhibiti Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Test Ban of Nuclear Weapons (CTBT)* na pia kuruhusu ufunguzi wa Kituo cha Kimataifa cha Udhibiti wa Mionzi Ayonisha katika Mazingira kutokana na Tanzania kuwa mojawapo ya nchi ambazo zinasifika kwa jitihada zake za Kimataifa za kuendeleza amani na utulivu.

Aidha, Kamati iliwekea maanani madhara na athari mbaya zilizowahi kutokea na zinazoendelea kutokea kutokana na matumizi ya silaha za nyuklia wakati wa vita kuu ya pili huko Hiroshima na Nagasaki, Japan na ajali mbaya ya mtambo wa gesi ya nyuklia huko Chinobil, Urusi na madhara yake. Hivyo ni vizuri nchi yetu ikachukua hatua zote kuzuia matumizi na majaribio ya silaha za nyuklia katika ardhi yetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ilizingatia kuwa Tanzania ni mwanachama wa Mkataba uitwao *The African Nuclear Free Zone Treaty, The Perindaba Treaty* ikiwa ni hatua ya kuiepusha Afrika kutokana na matumizi ya silaha za nyuklia.

Mheshimiwa Spika, kutokana na maelezo haya ambayo yamezingatia Mkataba wa *CTBT,* Kamati inaafiki kuwa ni vema nchi yetu kuwa kwenye mtandao wa kufuatilia mlipuko wa nyuklia *(International Monitory System)* ambayo manufaa yake ni pamoja na nchi yetu kupata takwimu za milipuko inayotokea duniani na madhara yake na kuweza kuchukua tahadhari kila inapowezekana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu itifaki ya ufunguzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kufuatilia Milipuko ya Nyuklia, Kamati yangu ilipata maelezo ya Serikali kuwa nchi yetu imechaguliwa kuwa mwenyeji wa kituo kimojawapo cha kufuatilia milipuko ya nyuklia kwa njia ya *Radio Nuclide Monitoring Station* kutokana na sababu za kijiografia.

Kwa njia hiyo nchi yetu itaweza kunufaika na taarifa zitakazopatikana kupitia kituo hicho na vituo vingine kwa ajili ya utafiti elimu, ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Spika, pia Kamati yangu ilifarijika kupata maelezo kuwa nchi yetu katika kuridhia Mikataba hii itaendelea kupokea misaada ya kiufundi inayohusu matumizi ya teknolojia nyuklia ambayo hutolewa na Shirika la Nguvu za Atomiki Duniani *(The International Atomic Energy Agency)* na pia itakuwa na sauti sawa kama Mwanachama wa *CTBTO* kwenye maamuzi yote yanayohusu matumizi ya Nguvu za Nyuklia katika vikao vya Kimataifa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuwasilisha maoni haya, sasa naunga mkono Maazimio haya yote mawili. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Azimio la kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia ikiwa ni pamoja na Azimio la kuridhia Itifaki inayoruhusu Ufunguzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kupima na Kufuatilia Viwango vya Mionzi Ayonisha katika Mazingira Chini ya Tume ya Kimataifa ya Kudhibiti Majaribio ya Silaha za Nyuklia *CTBTO*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naunga mkono Maazimio haya yote mawili yaliyowasilishwa kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatambua na kuelewa kwamba matumizi yasiyo salama ya silaha za nyuklia yanapotumiwa hapa duniani kwa kweli hayajali cha rangi, kabila, dini wala itikadi ya mtu. Kwa misingi hiyo kila mtu mwenye hekima na busara ni lazima akubali baada ya kuzingatia athari ambazo zinatokana na matumizi ya silaha hizo.

Mheshimiwa Spika, naelewa kwamba Mheshimiwa Waziri ametaja hasara za matumizi ya silaha za nyuklia zinaeleweka. Lakini pengine kwa niaba ya Kambi ya Upinzani nirudie tu kidogo athari hizo ili tuweze kuelewana vizuri. Ni kwa nini na sisi tumeweza kuunga mkono moja kwa moja Tanzania kuridhia Mkataba huo na Itifaki hiyo. Mheshimiwa Waziri ameainisha athari za kimazingira ziko athari kwa viumbe na binadamu.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba mwana-saikolojia mmoja alisema, "kama kuna wanyama ambao wana unyama zaidi kuliko wanyama wengine basi ni binadamu." Nasema hivyo kwa sababu ukijiuliza mpaka mwaka 1963 kama kwa mujibu wa teknolojia na sera zilizokuwepo vita ya nyuklia ingepiganwa kwa muda wa saa moja, basi watu wapatao milioni 300 wangeweza kuuawa kwa muda wa saa moja, na ukizingatia tatizo la matumizi makubwa ya kutengeneza na kujilimbikizia silaha ya nyuklia.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba sehemu kubwa ya fedha ambazo zingetumika katika afya, katika kilimo, katika kuendeleza jamii na ustawi wa wananchi na ustawi wa mwanadamu duniani sehemu kubwa imetumika katika matumizi ya silaha za nyuklia.

Mheshimiwa Spika, silaha hizo si kwamba zikitumika zinaweza kuondoa ukame, siyo kwamba silaha hizo zikitumika zinaweza kutibu magonjwa kama UKIMWI na silaha hizo si kwamba zinatumika kumdhibiti simba ama chui au mnyama mwingine yeyote, silaha hizo zinatumika kwa ajili ya kumdhibiti binadamu. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo ndiyo tunasema kwamba kuna athari kwa binadamu, na kwa misingi hiyo tunaona kwamba Azimio hili na Mkataba huu ni muafaka kabisa na sisi kama Taifa; na kwa kuwa hatuna silaha hizo tunadhani ni muhimu tuuridhie ili kuweza kulinda ustawi wa binadamu duniani kote.

Mheshimiwa Spika, athari za kiuchumi tukirejea katika historia mashindano kwa kweli ya silaha za kinyuklia pengine wachambuzi wengine wanaweza wasilione hilo, lakini kuporomoka kwa *Soviet Union* huwezi ukakutenganisha na kujilimbikizia silaha za kinyuklia, kwa sababu waliachana na mambo ya kimsingi ya ujenzi wa uchumi kwa kutumia fedha walizokuwa nazo na teknolojia waliyokuwa wamefikia

wakajilimbikizia silaha za nyuklia katika mashindano yao pengine na Marekani na kusambaza silaha zile katika nchi ambazo zilikuwa zinapingana vita pengine ambayo haikuwa na msingi. Kwa hiyo, kwa upande wa kiuchumi hilo waweze kuliona kwamba nchi zozote ambazo zingependa kujiingizia katika mashindano hayo kwa njia moja ama nyingine zitawaathiri watu wake katika misingi ya kiuchumi na tumeitaja hiyo *Soviet Union* ya zamani kama mfano.

Mheshimiwa Spika, pengine na Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kinachoendelea katika Korea ya Kaskazini wote mnaelewa miezi iliyopita vitisho vilivyokuwepo kati ya Korea ya Kaskazini na Marekani tunaelewa katika idadi ya watu, tunaelewa kwa upande wa Sayansi na Teknolojia, tunaelewa katika nguvu za kiuchumi, nguvu za kijeshi Marekani ni Taifa kubwa. Lakini kwa sababu ya kujilimbikizia silaha ambazo ingawa hawajatangaza rasmi kama wanazo silaha, lakini inaaminika wanazo Korea Kaskazini imeweza kutisha Marekani. Lakini hilo tu si suala la ubabe wala kuonyesha uanaume wa Taifa hilo la Korea Kaskazini isipokuwa wote tunaelewa kwamba wakazi zaidi ya milioni 3 mpaka 6 wa Korea ya Kaskazini wanakabiliwa na njaa na pengine wengine wanalala bila kula. Sasa mtu anaweza akajiuliza Taifa ndogo lenye watu milioni 23 kuweza kulitisha Taifa kubwa kama Marekani, lakini wakati huo huo haliwezi kujilisha. Kwa hiyo, huo ni mfano mwingine unaonyesha zaidi kwamba matumizi na tamaa ya kujilimbikizia silaha za nyuklia zinaweza zikaathiri afya na ustawi wa wananchi wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tunaangalia kwa sababu labda pengine za kisiasa wakati ule *Soviet Union* imejilimbikizia silaha pamoja na Marekani vilikuwepo vitisho na dunia ilikuwa imegawanyika katika kambi ambazo Mataifa mengine kwa kupenda ama kutokupenda yaliweza kwenda ama Mashariki ama Magharibi, kitu ambacho ni dhahiri kwamba hiyo ilikuwa na athari ambazo ni chanya na athari ambazo pengine zilikuwa ni hasi. Sasa itategemea mtu anachambuaje lakini tunavyoelewa ni kwamba baada ya kuvunjika kwa *Soviet Union* kumekuwepo na demokrasia na baadhi ya nchi hata kule wanakokuwa wanapingana kama Angola, Msumbiji na kwingine wameweza kufika katika hatua ya maridhiano kitu ambacho tunadhani sisi pengine kwa Afrika inatupeleka kwenda katika hali nzuri. Ukiacha sasa zile athari ambazo pengine ni hasi.

Mheshimiwa Spika, tukizingatia hayo tumekwisha kuona kwamba kwa misingi hiyo jamii ingeweza kuathirika na kama tulivyosema kwamba Tanzania wataungana katika kuwa moja ya nchi ambazo zitashiriki katika Kituo cha Udhibiti wa hii Mionzi Ayonisha. Ni kitu ambacho ni kizuri kwa sababu tumekwisha kuelewa wote kwamba mionzi hiyo ina athari kijamii. Kwa hiyo, kwa misingi hiyo Azimio hili na wale waliolianzisha tunawapongeza na ndiyo maana tunasema tunaunga mkono Serikali ya Tanzania kuridhia na kuwa mmoja kwa wale wote walioridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pengine ni ushauri kwamba wakati Tanzania inaridhia na kujiunga pengine kwa kutumia ushawishi wake hata kama ni mdogo iungane na nchi nyingine ili kuweza kuzishinikiza nchi ambazo tayari zilikwisha kutengeneza na kujilimbikizia silaha hizo waweze kuzipunguza ili tuweze kufikia ulimwengu usiokuwa na silaha za nyuklia. Nyuklia *Weapon free World.* Zipo juhudi za Taasisi na Vyombo mbalimbali vya Kimataifa vinafanya jitihada hizo.

Mheshimiwa Spika, vilevile tunazidi kutoa rai na maoni kwamba Tanzania vilevile ijiunge na wale wenye nia njema ya kuhakikisha kwamba nchi nyingine ambazo hazijapata teknolojia ya nyuklia kwa ajili ya silaha waweze kuzishinikiza zisifanye hivyo. Japo tunaelewa kwamba hatua hizo lazima zichukuliwe kwa ufundi na kwa ustadi na kwa hekima zaidi, kwa sababu wale waliokuwa na silaha kama Marekani wangependa kuendelea kutengeneza silaha nyingine.

Mheshimiwa Spika, ziko taarifa kwamba Rais George Bush tangu alipoingia madarakani amekuwa akijaribu kushawishi na kutengeneza silaha fulani za aina ya nyuklia kufuatana na eneo analotaka kulipinga au kama ni kutoboa miamba ama kitu kingine.

Kwa hiyo si kwamba kuzuia huko kumekoma bado kuna wengine ambao wanadhani watafute namna bora na teknolojia bora nyingine ya kuendelea kutengeneza silaha za nyuklia, kitu ambacho huenda kikasababisha hisia za kwamba na wengine nao watengeneze, na tukifikia hatua hiyo tunasema wale walio na silaha hizo waziharibu. Kwa sababu tunajua kuendelea kuwa nazo kunawafanya Mataifa mengine ambayo pengine kwa ajili ya teknolojia na kukuza uchumi kwao kutawafanya pale watakapokuwa

wameridhika kwamba uchumi wao unaenda vizuri na wamejilimbikizia fedha nyingine wakashawishika, kwa sababu wana fedha za ziada kuweza kutengeneza silaha za nyuklia. Kwa sababu kama dunia anaachiwa mtu mmoja kwa sababu ya kuwa nazo anawatisha wengine, basi hili haliwezi kutufanya kwamba hata yule aliyezuiwa anaweza akakaidi na kuweza kufanya hivyo. Ndiyo maana tunasema kwamba wote kama silaha zote zitaharibiwa tutakuwa na uhakika kwamba Mikataba hii haitaweza kukiukwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni dhahiri kwamba Kambi ya Upinzani inaelewa na wote tuliomo humu ndani ya Bunge tunaelewa kwamba kama Taifa moja ama Mataifa mawili yamekaidi kufuata Maazimio ya Umoja wa Mataifa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa yakaweza kuchukua hatua. Sasa wale ambao wana fedha za kuweza kufanya hivyo wanaweza wasiwaamini wale na wao wakaanza kujilimbikizia silaha. Kwa misingi hiyo tunaomba kwamba tunaporidhia tusiishie kwenye kuridhia bali mazungumzo yaendelee ili kuweza kuhakikisha kwamba wale wote walio na silaha hizo wanaziangamiza, na juhudi hizo tunadhani Tanzania ina heshima yake katika Umoja wa Mataifa hata kama si Mwanachama wa kudumu, lakini ina ushawishi wa aina fulani. Kwa hiyo, wakishirikiana na wengine tunaweza tukafika mahali tukaharibu silaha hizo na kuzizuia kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwamba tunaunga mkono Itifaki hii na Azimio hili na tunawashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninashukuru kunipatia nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu katika hili Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Udhibiti wa Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test - Ban Treaty).*

Mheshimiwa Spika, naliunga mkono Azimio hili asilimia mia moja na kwa kweli Azimio hili ni muhimu sana kwa Taifa letu la Tanzania na duniani kote kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hasa kinachohitajika ni ukweli kwa Mataifa haya ya Wananchama. Suala tunaloliridhia ni suala ni nzito kwa Taifa letu na Ulimwengu kwa ujumla. Na kwa kweli sasa hivi pamoja na maradhi yanayozungumzwa kwamba ni janga kubwa linaloathiri dunia. Lakini masuala ya silaha za nyuklia hata tukiangalia mfano wa Vita hivi vya Iraq vya hivi karibuni hata vile vya Afghanistan hata shutumu baina ya Korea ya Kaskazini ile na Marekani watu wana hofu kutokea janga kubwa sana katika ulimwengu kutokana na silaha hizi za nyuklia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mataifa haya Wanachama tungetaka cha msingi cha mwanzo kuwa wakweli juu ya Maazimio kama haya, pamoja na Mataifa makubwa ya dunia pamoja na Umoja wa Mataifa wenyewe ambao unasimamia majukumu haya.

Mheshimiwa Spika, nikisema ambacho kimezungumzwa katika Azimio hili. Nasema Azimio hili ambalo tunataka kuliridhia kwamba Tanzania ni moja ya nchi zinazoendelea duniani na nchi mwanachama wa Umoja wa Mataifa, sasa mimi nataka niulize je, uanachama wetu una sauti? Kama Mwanachama kunatakiwa mchango fulani uwe unatoa siyo wa fedha je, tuna sauti, na kama tuna sauti je, inasikilizwa kwa kiasi gani? Kwa sababu tumeona vita hivi vilivyotokea vya Iraq kwa shutuma kwamba imeonekana labda ina silaha za maangamizi. Lakini sasa hivi tunaona wakubwa hawa wanakiri kwamba zile taarifa za kijasusi za kwao hazikuwa sahihi. Je, kama wanachama tunaweza kuwalazimisha vipi Mataifa haya kuthibitisha ile shutuma ambayo waliisababisha hata dunia kuwa na hofu kwamba itatokea vita kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa vita vilivyopingwa Iraq vimesababisha janga kubwa sana kwa watoto, akinamama na vijana. Kwa hiyo je, kama Taifa na sisi ni nchi mwanachama tuna sauti kiasi gani katika uanachama wetu katika Azimio kama hili?

Mheshimiwa Spika, lingine katika Azimio hili ni kuwa nchi zote duniani zinakabiliwa na matatizo ya matumizi yasiyo salama wala ya amani ya nishati ya nyuklia na utengenezaji wa silaha za nyuklia. Je, Umoja wa Mataifa kama imekiri hili nchi mwanachama itamaliza vipi tatizo hili?

Mheshimiwa Spika, tunachokizungumza ni kitu kizito na isiwe utengenezaji wa silaha za nyuklia hata lugha kwa sababu tumeingia katika vita kwa shutuma tu za kauli za Marekani kwamba Iraq ina silaha za maangamizi. Dunia imeangamizwa kwa lugha tu. Hata kauli tu zinaweza kuangamiza umma.

Kwa hiyo masuala kama haya Umoja wa Mataifa yaangaliwe pengine lugha zinaweza kuangamiza umma kuliko hata hizi silaha. Kwa sababu wenzetu walitafuta sababu ya kuingia vitani wakasema Iraq ina silaha za maangamizi na tumeona wenzetu walivyoangamia kule Iraq. Inawezekana teknolojia hiyo ya vita vya pili vya dunia iliyoainishwa kwamba ndizo hizi silaha zilizoonyeshwa za kinyuklia. Je, teknolojia hii mpya iliyoingia sasa hivi, hizi silaha ambazo anamiliki Marekani na Mataifa mengine hazimo katika zile *agenda* za nyuklia? Kwa sababu tukiangalia kama zile ndege *DFT II.*

Mimi mara moja vile vita vya mwanzo vya Iraq, wakati vinatokea ule mgogoro wa Iraq mwaka 1991, mgogoro uliotokea baina ya Marekani na Urusi ni pale kiongozi wa Urusi wakati ule alipokuwepo akamjulisha Saddam Hussein kwamba vita vyako leo saa nane usiku unashambuliwa na Marekani na Mmerekani akaiona unamzidi kidogo anatumia silaha zito kama alivyozitumia. Na halafu na ndege yake moja inabeba mabomu yale kama 10, ambapo bomu moja linaweza kuiangamiza Iraq likawa jangwa milele.

Sasa kama kauli hizi zilitoka za kitaalamu na nchi kama Urusi kumwarifu Iraq mwaka ule 1991, hivi itakuwa kweli Marekani hana silaha hizi za maangamizi! Kwa hiyo, vilevile Umoja wa Mataifa uyasimamie Mataifa makubwa ndiyo tutaweza kufanikiwa haya.

Mheshimiwa Spika, nalisemea hili kwa sababu Iraq kilichowaponza wenzetu ni uchumi na sisi nchi yetu ni mwanachama na ni nchi ambayo inaendelea. Kwa hiyo, tunakuwa na hofu tutakapokwenda kwenye uchumi wa juu huko mbele ya safari tunaweza tukaingia kwenye majanga ambayo yamewakuta wenzetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili nataka tuliangalie sana Mheshimiwa Waziri atuthibitishie kwamba ule utafiti ulioainisha zile silaha za nyuklia za wakati huo je, hii teknolojia iliyoingia hii miaka ya karibuni baada ya vita vyan pili vya duni a je hakuna silaha ambazo zimetengenezwa kwa kiwango kidogo sana, lakini zina nguvu sawasawa na silaha za nyuklia. Tumeona juzi pale Iraq.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo namwomba Mheshimiwa Waziri anitoe wasiwasi tunaambiwa kuwa Baraza Kuu la Umoja la Mataifa lilipitisha Mkataba wa Kimataifa wa kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia *The Comprehensive Nuclear Ban Treaty* mwaka 1968. Sasa hapa tangu mwaka 1968 mpaka leo je, Umoja wa Mataifa umefanya tathmini kiasi gani?

Je, nchi wanachama zinajulishwa au zinashirikishwa? Kama tutakuwa tunafaidika na hayo, nataka niwathibitishie kwamba tutakuwa tumefaidika na Azimio hili. La! kama tunaazimia Azimio kwa kuhofia kwamba majanga haya yatalikuta Taifa letu itakuwa bado hatujafanya jambo la msingi kwa ulimwengu huu wa leo. Kwa sababu kama Taifa tuyasaidie Mataifa ya mwenzetu ili nayo yaishi kwa usalama.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimio hili. Namwomba Mheshimiwa Waziri anifafanulie hayo machache ili na mimi niweze kuelewa na kuendana na hali ya dunia . Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA SAYANSI, TEKNOLOJIA NA ELIMU YA JUU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi nyingine ili niweze kujumuisha na kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Kwanza, Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii, tunamshukuru sana na Kamati yake, kwa ushauri waliotupatia katika Kamati na kwenye Bunge lako Tukufu, tunazipokea pongezi zake na vile vile ushauri ambao ameutoa.

Kwa upande wa Kambi ya Upinzani Mheshimiwa Benedicto Mutungurehi maoni yake tunayashukuru kuyapata na tunashukuru kwamba ameunga mkono Maazimio haya. Ametupatia maelezo zaidi kuhusu athari za nyuklia hasa athari zinazohusu uchumi na ustawi wa jamii.

Tunakubaliana naye kwamba athari hizo zipo na mifano ipo ya nchi ambazo zinatumia fedha nyingi sana katika kutengeneza silaha hizo. Nchi zenyewe ni nyingi ni pamoja na Marekani yenyewe inapata athari kubwa sana kwenye uchumi wake katika kutengeneza silaha kama hizi. Ila wao ni wajanja kwa sababu kama mnavyofahamu uchumi wao unategemea *deficit financing* kutoka Mataifa mengine.

Kwa hiyo, hawasikii moja kwa moja ule uzito wa uchumi wao unavyokwenda. Lakini ni kawaida kabisa kwamba utengenezaji wa silaha unaleta athari kubwa sana. Vitisho vinavyotokana na athari nyingine kukaa katika vitisho, amani inaonekana kwamba sasa hivi haiwezi kuendelea kuwapa amani kwa msingi wa vitisho, kwa sababu ya kitisho ndiyo sababu inakuwa amani.

Wakati fulani katika mazungumzo ya Umoja wa Mataifa kulikuwa na neno linaitwa *MAD, Mutual Assured Distraction.* Sasa tulipokuwa na sehemu mbili zenye silaha kali sana za nyuklia upande wa Marekani na wenzake na upande wa Mashariki ukiongozwa na *Soviet Union,* wakati ule amani ilipatikana *through this press percept* inaitwa *the Mutual Assured Distraction* waliogopana kwa namna hiyo. Lakini matokeo yake ndiyo hivyo miaka hiyo hatukuendelea sana katika sehemu zingine za ustawi wa jamii.

Kwa hiyo, nakubaliana kabisa na mawazo ya Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi kwamba tuna sababu za kutosha kabisa za kuogopa maendeleo katika silaha hii na kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba silaha hizi zinatoweka na haziongezwi.

Rais George Bush na washirika wake wamejitahidi sana kuhakikisha kwamba Mikataba ya aina yoyote hii haifanikiwi hasa huu *CTBTO* ingawa wameishauwekea saini, lakini bado hawajauridhia.

Wenyewe wana mawazo tofauti na katika Mkutano wa mwaka jana wa Vienna ambao ulikuwa unajadili *Article 14* ya Mkataba huu Marekani hawakwenda, lakini vilevile India haikwenda na Korea Kaskazini hawakwenda na wote hawa ndiyo ambao Bunge lako Tukufu baada ya kuridhia Mkataba huu Serikali inatuomba kuwashawishi waweze kuingia katika Mkataba huu. Wanabakia nchi 12 ambazo zikiridhia basi Mkataba unaanza kutumika na hawa nchi 12 ndiyo ambao wanavuta miguu yao na wanatuchelewesha. Kama nilivyosema nchi nyingi zimeisharidhia na zimekwishaweka saini.

Lakini katika Mkataba huu wale watu wenye silaha hizo au wenye *capabilities* ya kuwa na silaha ndiyo lazima kwanza waweke saini na vilevile waridhie. Wamebakia nchi 12 tu nao tunawashawishi hao maana yake tuna mvuto wa kuweza kuwashawishi ili waweze kuridhia vilevile Mkataba huu.

Mheshimiwa Janet Kahama kwa maandishi tunamshukuru kwa kushiriki naye ametuomba Serikali baada ya kuridhia Mkataba huu tutumie nafasi yetu katika Umoja wa Mataifa na katika Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa tutumie sasa mvuto wetu na uzeofu wetu kuweka shinikizo na kuweka ushawishi kwamba watu wengi waingie na kuridhia Mkataba huu.

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali ametuasa na kutushauri katika mambo mbalimbali. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Omar Mjaka Ali kwamba Tanzania inajulikana kwa mvuto wake Kimataifa kuweza kushawishi na tumeshawishi mfano ni mapambano ya kuikomboa Afrika.

Hapa Tanzania ilikuwa katika mstari wa mbele kabisa mpaka Kamati ikawekwa ya Umoja wa Taifa, mpaka nchi zote zimekombolewa. Hata ule msingi wa Kimataifa kwamba *of self-determination* kwamba nchi ziweze kujiamuliwa zenyewe ni Tanzania ambayo ilikuwa katika mstari wa mbele.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali asiwe na wasiwasi bado mvuto wetu na ushawishi wetu Kimataifa ni mkubwa sana na hii inajulikana na kuwekwa mkazo na Bunge lako Tukufu ndiyo linalotupeleka nje, sauti ya Tanzania inasikilizwa sana. Hata Kambi za Upinzani mnaona mnapokwenda nje, ukisema unatoka Tanzania una mvuto mkubwa. Kwa hiyo, hili sina shaka kabisa katika upande huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ndiyo maana tunaomba Bunge lako Tukufu liweze kuridhia Mkataba huu na uweze kupelekwa tukaongeze sisi nafasi yetu, kule sisi kutokuwemo mle ndani pengine ungelikuwa ni mvuto *negative* kidogo kwamba kwa nini Tanzania bado inavuta miguu yake.

Tulikuwa tunafikiria sasa tumeamua kwamba faida ni kubwa sana. Kwa hiyo, kuingia kwetu watasema aah naam hata Tanzania sasa imeona faida yake.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo haya, kwa heshima naomba kutoa hoja kwamba sasa Maazimio haya ambayo yametolewa mbele ya Bunge lako Tukufu, yaweze kuridhiwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclear Test - Ban Treaty (CTBT)***

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuzuia Majaribio ya Silaya za Nyuklia liliridhiwa na Bunge)*

**Azimio la Kuridhia Mkataba kuruhusu Ufunguzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kupima na Kufuatilia Viwango vya Mionzi ya Ayonisha Katika Mazingira Chini ya Tume ya Kimataifa ya Udhibiti wa Majaribio ya Silaha za Nyuklia *(The Comprehensive Nuclea - Test Ban Treaty Organization (CTBTO)***

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuruhusu Ufunguzi wa Kituo cha Kimataifa cha Kupima na Kufuatilia Viwango vya Mionzi Ayonisha liliridhiwa na Bunge)*

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

**Muswada wa Sheria ya kufanya Marekebisho katika Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya mwaka 1988 wa mwaka 2004 *(The Parliamentary, Immunities, Powers and Privileges (Amendment) Bill, 2004)***

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwanza na mimi nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa kwake kuwa mwenzetu katika Bunge hili. *(Makofi)*

Baada ya hapo naomba nijielekeze kwenye Muswada ambao naamini Waheshimiwa Wabunge wameuona. Hasa kwa ufupi sana Muswada huu umeingiza Ibara mpya katika Sheria mama yaani Sheria namba 3 ya mwaka 1988 mabadiliko mengine yatakuwa katika vipengele vinane kama nitakavyofafanua kwa ufupi na marekebisho yanakuja sasa hivi yatagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kwanza mabadiliko yamefanywa katika sehemu ya kwanza kifungu cha pili cha Sheria mama kwa kuongeza maneno mapya yafuatayo katika maeneo yake. Maana yake kwanza ni *code of contact* kuwa ni Kanuni za Maadili zilizotungwa kwa mujibu wa kifungu 12(a) cha Muswada huu.

Pili, kufutwa kwa maana ya zamani ya neno *Committee* na kulipa neno hilo maana mpya inayohusisha Kamati nyingine za Bunge iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara 89 ya Katiba na kuhusisha pia Kamati za Kudumu za Bunge.

Tatu, kuongezwa kwa neno *Minister* kuwa ni Waziri anayekasimiwa madaraka kusimamia masuala ya Bunge kwa Kiingereza ni *Minister of Parliamentary Affairs.*

Mheshimiwa Spika, pili Sheria mama inafanyiwa marekebisho katika kifungu cha tatu na kuongeza kifungu kipya ambacho kinasomeka kama Ibara ya 3(a) kinachotoa maelezo na masharti ya matumizi ya Bendera na bahati nzuri Mheshimiwa Spika, Bunge lako limeishaingiza masharti haya kwenye Kanuni tayari.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwepo Bendera ya Bunge ni jambo ambalo limekuwepo kwa muda mrefu, lakini utekelezaji wake umechukua muda mrefu kutokana na maandalizi ya utengenezaji wa hizo Bendera ambao ulifanyika nje ya nchi. Zimetengenezwa na Waheshimiwa Wabunge mlionyeshwa na Vyombo vya Habari wameishaonyeshwa. Bendera za aina tatu, Bendera ya kutunika kwenye mlingoti, bendera ya mezani na ile ya kuweka kwenye gari la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukamilika kwa utengenezaji wa bendera ya Bunge bado ilionekana kuwa isingekuwa busara kuanza kuzitumia kutokana na ukweli kuwa masuala kadhaa yahusuyo bendera hiyo yalikuwa bado hayajawekewa utaratibu wa kisheria. Kazi ya kifungu hiki katika Muswada huu ni kuweka taratibu hizo na taratibu hizi narudia tena ni kama zile zile zilizowekwa kwenye kanuni yetu na zimefafanuliwa vizuri zaidi.

Labda kwa kurudia tu ni kwamba kama mtakavyoona kwenye Muswada kwamba imezingatia maeneo ambayo bendera itatumika ile ya mezani na ile ya ofisini na ile ya kwenye gari na pengine ufafanuzi zaidi ulitolewa na Makamu Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kanuni juu ya namna ya kuitumia hata ndani ya gari kwamba Mheshimiwa Mbunge lazima awepo kwenye gari ana bendera inakaa kushoto mwa gari na muda wa kuitumia. Maelezo yote yanafafanuliwa vizuri kwenye kanuni na kwenye sheria hii.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 12 cha Sheria Mama kimefanyiwa marekebisho na kuongeza vifungu vidogo vya 5 na 6 mara baada ya kifungu cha 4. Kifungu kidogo cha 5 kinahusu Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maombi toka kwa Mheshimiwa Spika juu ya hatua zilizochukuliwa na Mahakama kutokana na mapendekezo ya Bunge au Kamati ya Bunge kama ilivyoelezwa katika kifungu kidogo cha 3. Kifungu kidogo cha 6 kinaeleza kuwa Mahakama yoyote inayotambuliwa kisheria ina uwezo wa kutoa hukumu juu ya kosa lililofanywa kwa mujibu wa sheria hii. Mwisho katika sehemu hii mabadiliko yamefanywa tena katika kifungu cha 12 cha Sheria Mama ambapo kifungu kipya cha 12(a) kimeongezwa ili kulipa Bunge uwezo wa kutumia kanuni zake kwa Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko mengine yamefanyiwa katika sehemu ya 3 amnbapo kifungu cha 20 cha Sheria Mama kimeboreshwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha 3 mara baada ya kifungu cha 2. Kifungu hiki kipya kinampa Spika uwezo wa kutupilia mbali ushauri utakaoonekana kuwa ni wa uongo na mhusika kustahili adhabu kama vile mtu aliyevunja sheria chini ya kifungu cha 122 cha *Penal Code.* Kifungu kidogo cha 3 cha Sheria Mama sasa kinakuwa kifungu kidogo cha 4 na kifungu cha 5 kimeongezwa ambacho kinamnyima shahidi yoyote kinga kama ilivyo katika kifungu kidogo cha 4 endapo ushahidi umekataliwa chini ya kifungu kidogo cha 3.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya 5 imefanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 30(a). Kifungu hiki kinatoa madaraka kwa Bunge kuwa na uwezo wa kupitisha Azimio la kutaka Mheshimiwa Spika, kuweza kumuonya Mbunge au kumsimamisha katika shughuli za Bunge kwa muda utakaoamuliwa. Kifungu hiki kimefanyiwa marekebisho kitawezesha sasa Mheshimiwa Mbunge aliyesimamishwa kazi kupata nusu ya mshahara, Kifungu cha zamani kilikuwa kinamnyima mshahara kabisa. Aidha, Bunge limepewa madaraka ya kumruhusu Mheshimiwa Spika, kumwita Bungeni mtu ambaye sio Mbunge kwa kosa atakalokuwa amefanya kwa mujibu wa sehemu ya 24 ya sheria hii.

Kifungu cha 31 kimerekebishwa kwa kuondoa kifungu cha maneno *"On conviction be liable to a fine not exceeding ten thousand".* Yalionekana mwishoni mwa sentensi na kuweka maneno yafuatayo *"On conviction be liable to a fine not exceeding five hundred thousand".* Madhumuni ya mabadiliko aya ni kubadili tu viwango vya faini kutoka shilingi 10,000 na kuwa shilingi 500,000 ili iendane na wakati. Aidha, kifungu kidogo cha 2 kimeongezwa kifungu kidogo hiki kinataja adhabu kwa mtu atakayetumia Bendera ya Bunge kinyume na kifungu cha 3(a).

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 32 cha Sheria Mama kimefutwa na badala yake kimewekwa kifungu cha 32 kinachotoa adhabu ya shilingi 3,000,000 au kifungo miaka 5 au vyote kifungo na faini kwa Mbunge atakayepokea rushwa. Narudia tena kwamba Mheshimiwa Spika, mwisho wa Muswada huu mtaona kuna jedwali ambalo linaonyesha picha ya bendera itakavyokuwa na bahati mbaya tumeweka ni *black and white* lakini rangi zote zinajulikana.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge naomba radhi kwamba marekebisho yamekwishatolewa tayari .

**WABUNGE FULANI:** Yako wapi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** Yanakuja, yanatolewa sasa. Naomba Waheshimiwa Wabunge wazingatie Muswada ule uliowasilishwa pamoja na marekebisho ya msingi hata kifungu kikubwa kilichoingizwa hapa ni kile cha Bendera ambacho kwanza tulishapitisha marekebisho haya yameshaingia kwenye Kanuni.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA - MWENYEKITI WA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii kwa niaba ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu marekebisho ya sheria kama ilivyotajwa na Mheshimiwa Waziri.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 70, kifungu cha 2 ya Kanuni za Bunge napenda kuchukua fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kamati yangu juu ya Muswada wa Sheria kufanya marekebisho katika Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge wa Mwaka 2004 *(The Parliamentary, Immunities, Powers and Privileges (Amendment) Bill, 2004)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Kamati yangu imeridhika na Muswada huu kwani umekuja wakati muafaka. Hata hivyo, Kamati ina ushauri katika maeneo kadhaa ili kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya 2 ya Muswada kifungu cha 2 Kamati inashauri kuwa tafsiri iliyotolewa kwa neno *"Minister"* iwe ni *"Minister responsible for Parliamentary Affairs"* badala ya ilivyo sasa kwani hakuna Waziri anayeshughulikia Bunge *(Parliament).*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa sehemu ya 3 katika kifungu cha 3(a), Kamati inapendekeza kifungu cha 3 kirekebishwe ili mamlaka ya kutunga kanuni za matumizi ya bendera ya Bunge yawe ni kwa Bunge lenyewe badala ya Waziri. Hata hivyo iweke wazi kuwa kanuni zitakazotungwa zisikinzane na sheria na matumizi ya sheria ya bendera ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya 5 kifungu cha 8 kidogo cha 2, Serikali inapendekeza kuwa Mbunge anapothibitika kukiuka sheria hii anaweza kusimamishwa ubunge kwa kipindi kilichotajwa kwa mujibu wa kanuni za Bunge. Aidha, Serikali inapendekeza kwamba Mbunge huyo aliyesimamishwa kazi ya Ubunge hatapewa mshahara wake wala marupurupu yoyote yanayoandamana na mshahara huo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa adhabu ya kusimamishwa Ubunge ni adhabu tosha. Kwa kuwa Mbunge ataacha tu kushiriki shughuli za Bunge, Bungeni lakini ataendelea kutekeleza majukumu yake jimboni. Kwa kuwa sheria mtu hawezi kuadhibiwa mara mbili. Kamati yangu inashauri kuwa kifungu hiki kirekebishwe, marekebisho yanayopendekezwa ni kuwa kwa kipindi ambacho Mbunge atakuwa amesimamishwa Ubunge atapokea nusu mshahara na nusu marupurupu yanayokuja pamoja na mshahara wake.

Mheshimiwa Spika, marupurupu ya *Sitting allowance* na ya kuja Bungeni atakuwa ameyakosa kwa sababu atakuwa hayupo. Lakini kama Jimbo *allowance* ni vizuri angepata nusu yake na vile vile nusu mshahara ili kumwezesha kuendelea kufanya kazi yake vizuri. Nashukuru na kuipongeza Serikali kwamba imepokea ushauri huu na punde hivi mmemsikia Waziri wa Nchi, katika Ofisi ya Waziri Mkuu akiwasilisha kama tulivyokubaliana.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu pia ilibaini mapungufu kadhaa yaliyojitokeza katika sheria hii lakini hayakuguswa na Muswada huu. Kifungu cha 4 kinaeleza kwamba, "Mbunge ana haki kuendesha mikutano ya hadhara akiwa jimboni kwake, Mamlaka husika ziwezeshe mikutano hiyo kufanyika bila matatizo. Aidha, kifungu kidogo cha 2 kinaeleza kuwa, "Mtu yoyote atakayezuia au kufanya vurugu katika mikutano hiyo atakuwa ametenda kosa na atastahili kushughulikiwa na mamlaka husika. Hata hivyo adhabu inayotakiwa kutolewa haijawekwa wazi".

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inaamini na ina ushahidi kuwa lakini na hii inaweza kuleta utata katika utekelezaji na kukwamisha haki kutendeka. Kwa hiyo, Kamati inapendekeza kwamba kifungu hiki kifanyiwe marekebisho na kuweka wazi adhabu kwa kosa lililotajwa la Mbunge kuzuiwa kufanya mkutano wake wa halali.

Mheshimiwa Spika, suala la Mbunge kutopeperusha bendera yake katika Manispaa za Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar lilijitokeza sana katika majadiliano ya Kamati. Aidha, Kamati imezingatia maoni na maombi ya Waheshimiwa Wabunge husika katika maeneo hayo kwamba bendera hiyo ni kitambulisho cha kuwepo kwa Mbunge katika eneo fulani la jimbo lake. Hivyo inapendekezwa kwamba Serikali ifikirie kumpa Mbunge huyo fursa ya kutumia bendera hiyo awapo kwenye shughuli rasmi za kikazi kwa mfano kwenye mikutano yake anapoongea na wananchi wake. Serikali ifikirie hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako kuwa Serikali imekubali mapendekezo mengi katika haya tuliyokuwa tumejadili ni matumaini yangu yale kuwa yale yatakayotakiwa kufanyiwa kazi na Serikali kadri tulivyoomba hivi nayo yatafanyiwa kazi na kanuni zetu kurekebishwa pale itakapoona inafaa na wakati muafaka wa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda nikushukuru sana kwa nafasi hii na nimshukuru sana Mheshimiwa William Lukuvi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu na hali kadhalika Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufafanuzi mzuri pamoja na wataalamu wake. Aidha, nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. Mzindakaya ambaye naye alishiriki pamoja na sisi katika kuchambua maeneo fulani. Lakini kipekee napenda niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati yangu ambao ningependa niwatambue kwa ajili ya rekodi Mheshimiwa Spika.

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Eliachim J. Simpasa | - | Mwenyekiti |
| Mhe. Maria D. Watondoha | - | Mjumbe |
| Mhe. Chifu Abdallah Fundikira | - | Mjumbe |
| Mhe. Athumani S. M. Janguo | - | Mjumbe |
| Mhe. Juma S. N'hunga | - | Mjumbe |
| Mhe. Hamad Mohamed | - | Mjumbe |
| Mhe. Abdulkarim E. H. Shah | - | Mjumbe |
| Mhe. Abdullatif H. Esmail | - | Mjumbe |
| Mhe. Cynthia H. Ngoye | - | Mjumbe |
| Mhe. Nimrod Mkono | - | Mjumbe |
| Mhe. Mwanne I. Mchemba | - | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| Mhe. Bernard K. Membe | - | Mjumbe |
| Mhe. Dr. M. R. M. Lamwai | - | Mjumbe |
| Mhe. Benedicto M. Mutungirehi | - | Mjumbe |
| Mhe. Ali Ameir Mohamed | - | Mjumbe |

Bila kumsahau Katibu wetu Bibi Nenelwa Mwihambi kwa kusaidia sana katika shughuli hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga hoja hii mkono na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA MASUALA YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maoni ya Kambi ya Upinzani juu ya *(The Parliamentary, Immunities, Powers and Privileges (Amendment) Act, 2004)*

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kukubaliana na Mheshimiwa Waziri na hasa Kamati yale mapendekezo au maombi ya Kamati ambayo yamekubaliwa, tunaishukuru Serikali kwa kukubali hilo.

Mheshimiwa Spika, *privileges* za Wabunge ningeomba Serikali iangalie *immunities and privileges* ambazo ziko kwenye Baraza la Wawakilishi ambazo zinampa Mbunge au Mwakilishi haki au *privileges* za kulindwa mpaka kwenye jimbo lake la uchaguzi. Hizi za kwetu sisi zinatulinda ndani ya Bunge tu lakini nje ya Bunge hazitupi ulinzi wowote.

Kwa hiyo tunashauri kwa sababu Mbunge asilimia 60 wa muda wake anautumia katika jimbo lake na ni asilimia 40 tu anatumia kwenye Bunge ni vizuri akapata *immunities and privileges* kama zile anazozipata katika Bunge akiwa kwenye jimbo lake la kazi. Hilo ndilo pendekezo la kwanza la Kambi ya Upinzani na hilo lipo katika *privileges and immunities* ya Sheria namba 5 ya mwaka 1984 ya Baraza la Wawakilishi. Tungeomba Serikali iangalie sheria hiyo ili katika nchi moja tusiwe na utaratibu tofauti. Kule Baraza la Wawakilishi wajumbe wanapata haki hiyo na huku hawapati.

Mheshimiwa Spika, pili katika ile *Privileges Act* ya Baraza la Wawakilishi kabla Mbunge hajakamatwa kwanza anatakiwa anayetaka kumkamata apate idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, havamiwi tu ovyo ovyo tu Mbunge. Kwa hiyo, Mbunge anapata kaheshima fulani fulani kidogo. Mimi ningefikiri ni utaratibu mzuri Mbunge kabla hajakamatwa basi angalau Serikali iwe na taarifa rasmi na iwe imetoa idhini kwa kupitia Mwanasheria Mkuu wa Serikali huyo mtu akamatwe, hiyo itatusaidia kwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu tunalopendekeza kwenye Kambi ya Upinzani ni hili suala la bendera katika *Municipalities.* Nafikiri kulikuwa na kilio hata cha Mheshimiwa Dr. Mahanga kwamba katika majimbo ambayo ni nje ya mji wa Dar es Salaam. Dar es Salaam kwa mfano ni mji mkubwa sana ukitoka tu ukiingia Kawe huonekani tena kama uko Dar es Salaam Mjini, sasa Mbunge katika mazingira hayo aruhusiwe kupepea bendera yake. Chukua Zanzibar ambapo kuna majimbo 13, sasa unasema majimbo yote 13 Wabunge pale wasipate haki ya kupepea bendera yao hata kama huko Rais Mheshimiwa Kissasi kule Dimani naye asiruhusiwe kupepea bendera haya hayana uhusiano na mambo ya mijini. Mimi nafikiri sheria ingeangaliwa yale maeneo ambayo Mbunge atakuwa kwa kweli anaonekana kama Mbunge katika maeneo yake huko basi aruhusiwe kupepea bendera si kumzuia kila mahali. Hilo lilikuwa ni jambo la tatu ambalo tungeomba Serikali ilitazame.

Mheshimiwa Spika, lingine tunashuhudia viongozi wanapokuja kwenye shughuli zao nje ya zile za Serikali wanachukua na bendera zao za Serikali. Lakini Mbunge anapokwenda katika shughuli zake za siasa tu chama chake kwa mfano anaambiwa huku bendera yako usitumie. Sasa nasema labda hapa kuna mgongano kidogo, Viongozi wengine wanaruhusiwa kutumia bendera zao mpaka kwenye shughuli zao za kisiasa na wengine wanazuiwa. Lakini na Mbunge ni mwanasiasa. Kwa hiyo, mimi nafikiri labda Mbunge katika shughuli zozote zile mradi yeye yuko katika shughuli rasmi basi aruhusiwe kutumia bendera yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya Kambi ya Upinzani inaunga mkono hoja hiyo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PHILLIP S. MARMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa hii fursa ya awali ili mimi nijadili Muswada huu wa Haki, Madaraka na Kinga za Bunge.

Lakini kabla ya hapo naomba nimshukuru sana Waziri kwa kutuletea Muswada huu wa kufanya marekebisho ya sheria hii ya mwaka 1988. Nichukue nafasi hii pia kuwatakia Wabunge wote kila la kheri na fanaka tele kwa mwaka mpya. Nampongeza Mheshimwa Makongoro kwa kuja tena katika nyumba hii, nawapongeza Wabunge waliochaguliwa kuingia katika Bunge la Afrika na *SADC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hakika mabadiliko au marekebisho yaliyoletwa na Mheshimiwa Waziri ni sehemu ndogo tu ya maudhui mazima ya sheria yetu ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge ya mwaka 1988. Hivyo mimi nitachukua muda mfupi sana kujadili maeneo muhimu yaliyopo katika Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni lile eneo la bendera. Mimi sina tatizo na eneo hili isipokuwa kuwahakikishia tu wananchi kwamba bendera hizi sio mbwembwe. Kwa kweli nchi yetu ni kubwa na Wabunge wote huwa tunasafiri kwa njia ya barabara, magari kwa ajili hiyo kutambulika ni njia moja ya kujisalimisha. Wenzetu katika nchi jirani Wabunge wanakuwa na walinzi zaidi ya watano, sita mpaka nane na ni gharama kubwa kwa Serikali. Nafikiri hii ni busara kubwa ili kujihakikishia usalama kwa kutumia bendera kuliko gharama ya walinzi kama ilivyo katika nchi jirani.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 5 ya Muswada inaongelea kuhusu namna ya kuwashtaki wale ambao wanakiuka sheria hii. Hii inanikumbusha shahidi ambaye alijaribu kumpiga Mbunge wakati wa shughuli za Kamati ya Bunge, wakati akihojiwa na taarifa alipopelekewa Mwanasheria Mkuu alikaa kimya hadi leo. Sasa bila shaka utaratibu mpya mtu yoyote ambaye anaweza kuhatarisha maisha ya Mbunge wakati akifanya kazi za Kamati anaweza akishughulikiwa na tukapata taarifa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni hii ibara ya 6 ya kutaka sasa tuwe na kanuni za maadili kwa ajili ya Wabunge. Fani yoyote ya heshima duniani inakuwa na kanuni za Maadili. Kwa maana ya sheria yetu na kazi zetu kwa kweli ni kazi ya heshima wananchi wametupa dhamana, wametupa imani ya kuwawakilisha kuongea kwa niaba yao katika nyumba hii kwa vile wao kwa wingi, wao milioni 35 na zaidi wasingeweza kukaa wakafanya maamuzi mazito kwa ajili ya nchi. Kwa hiyo, hii ni heshima ya pekee na heshima hii lazima sio tu tena ithamini, lakini heshima hii lazima izingatie maadili ambayo yanafanana na uzito wa kazi zenyewe. Kwa hiyo nashukuru sana kwa mara ya kwanza kwamba sasa tutakuwa na kanuni za maadili kwa ajili ya Wabunge. Hatukuwa nayo mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia dunia inakwenda haraka sana katika maeneo ya teknolojia na uchumi; nadhani ile ibara ya 10 ya Muswada huu kwa kweli ingelikuwa ndiyo sehemu ya maadili yenyewe, kwamba Mbunge hawezi akanunuliwa na mtu yeyote kirahisi akaja kuongea kwa niaba yake. Hapa nina maana ya pia Kampuni au mtu binafsi mwenye maslahi na jambo ambalo linajadiliwa Bungeni wakati wowote ule.

Mheshimiwa Spika, lingine nafikiri ni lile la kusema kwamba wakati tunaletewa Muswada huu nadhani ni wakati muafaka wa kuwakumbusha wananchi na Waandishi wa Habari juu ya umuhimu wa kuwa na sheria madhubuti ya haki, Madaraka na Kinga za Bunge. Kwamba sheria hii sehemu muhimu ya kanuni na uendeshaji wa shughuli za Bunge. Sheria hii inakaza kanuni zetu na uendeshaji wa shughuli za Bunge na inatakiwa iheshimiwe na mtu yoyote yule ikiwa ni pamoja na Waandishi wa Habari kwa sababu sio pia kwa ajili ya mbwembwe ni kwa sababu kwa ajili ya umuhimu kuona kazi nzito inayofanywa humu.

Mheshimiwa Spika, sasa historia inalitambua hili Bunge au *Parliament.* Katika historia, sio lazima iwe tulivyokaa, inaweza kuwa mkutano wa Machifu, Maaskofu, mkutano wa watu mashuhuri ndio Bunge na kanuni na taratibu huu kwamba ni mkutano muhimu sana na lazima uongozwe na kanuni na sheria ambazo zinajulikana. Kwa hiyo, ni wakati bora na ni fursa ya kuwakumbusha Waandishi wa Habari na wananchi umuhimu wa kinga hizi.

Mheshimiwa Spika, kinga hizi zinahusika hasa na shughuli ambazo tunazifanya ndani ya Bunge kwa maana ya jengo hili na maeneo yanayolizunguka jengo hili. Lakini tumekwenda mbali Mheshimiwa Hamad Rashid alikuwepo na mwaka wa 1988 kwamba kinga kufikishwa hadi kwenye majimbo sio traditional halikuwepo hata kwenye mtiririko mzima wa Muundo wa Kanuni na Sheria za Kinga na Haki za Bunge.

Wakati ule tulikuwa na chama kimoja lakini dhana hii tulijadili kama wale waliokuwepo watakumbuka tulijadili kwa muda wa vikao viwili. Kikao cha kwanza ilishindikana kupitisha Muswada mpaka kikao kingine, sehemu kubwa ilikuwa hii na ilikuwa chama kimoja ndani kulikuwa na mvutano kati ya nani, chombo gani, taasisi gani nzito kati ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi na Bunge. Leo nadhani wenzetu wa upande wa Upinzani wangetumia vizuri zaidi eneo hili. Tunasisitiza yale aliyoyasema Mwenyekiti wa Kamati kwamba sheria iko kimya wakati wa kuchukua hatua kwa yule ambaye anaingilia mkutano wa Mbunge katika jimbo lake.

Mheshimiwa Spika, hapa pia tungekumbushana dhana ya Kinga na Haki na Madaraka ya Bunge inataazamwa nasi. Kuhusiana na vyama vya siasa vilivyomo humu iwe Chama Tawala au iwe ni Chama cha Upinzani hapa uasi kwamba sio kwa maana ya kwenda porini, kuasi kwa maana ya kutofautiana kimawazo na chana. Matamshi ya Mbunge Bungeni hayatahojiwa mahali popote hata kwenye kikao cha Kamati Kuu ya chama chake.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka maamuzi ya rafiki yako Mheshimiwa Ndebele aliyekuwa Spika wa Bunge la Zimbabwe ambapo *ZANU-PF* kabla ya Uchaguzi wa mwaka 2000 kilikuwa chama chenye nguvu sana. Kilikuwa na Mbunge mmoja wa Upinzani. Nadhani wala sio wa upinzani sana, ajitegemea akitoka jimbo moja katika Jiji la Harare, lakini wengine wote walikuwa *ZANU-PF.* Baadhi yao waliasi katika masuala fulani fulani ndani ya Bunge. Kamati Kuu ya *ZANU-PF* ilipotaka kuwachukulia hatua Spika alikataa na kuiarifu Kamati Kuu ya *ZANU-PF* kwamba uwezo waliokuwa nao ni hadi mwisho wa maisha ya Bunge mwaka 2002 wasipewe fursa ya kusimamishwa kama Wabunge.

Kwa hiyo, hii ni haki na kinga ya hali ya juu sana. Hapa nadhani kanuni itaniruhusu inanipeleka mahali alipo mwenzetu Mheshimiwa Asha Ngede. Wenzetu wa Kambi ya Upinzani nadhani wanajenga hoja kwamba Asha Ngede kwa kuunga mkono hoja ya Bajeti ya mwaka 2001. Ikiwa ni yeye mwenyewe tu kutoka kwenye Kambi ya Upinzani kuunga mkono Bajeti, Alikuwa amekosa? Hajakosa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Asha Ngede analindwa kwa asilimia mia moja na Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge. Sio tu desturi lakini pia ni Sheria ya mwaka 1988. Kwa hiyo, ni makosa makubwa sana kumnyima haki zake kutokana na msimamo wake ndani ya nyumba hii. Kusiwe na kisingizio cho chote kwa sababu katika Bunge hili tunafahamu rekodi ya Mbunge Kambi ya Upinzani ambaye alikataa kujiunga na wenzake kupinga Bajeti na Muswada wa *NMB.* Sasa isiwe ni nongwa huyu alikuwa anatumia haki zake na analindwa na sheria na mila za Kibunge. Kwa hiyo, ni makosa makubwa sana kumwona kama muasi, uasi unaruhusiwa. Hata Mbunge wa CCM anaruhusiwa kuasi. Haki ya chama chochote sasa juu ya Mbunge wa aina hii ni kutokana Uchaguzi Mkuu kwenye majimbo sio vinginevyo. Kwa hiyo, visingizio vingine vyote vyote vile kwa mambo yoyote yale ambayo Mbunge ameyatenda katika eneo hili yasitumike kumnyima haki zake za Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni eneo muhimu na pana sana katika uendeshaji wa shughuli za Bunge na mimi nimeona nitumie fursa hii leo ya kuwakumbusha wenzangu, wananchi na Waandishi wa Habari kwa ujumla juu ya umuhimu wa Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge katika uendeshaji bora zaidi wa Bunge. Ahsante kwa kunipa nafasi hii naunga mkono Muswada. *(Makofi)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nizungumzie kuhusu *Parliamentary Powers and Privileges Amendment* iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, katika mchango wangu ninachofahamu ni kwamba tuna *pillars* tatu ambazo ni Bunge, *Executive* na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ukienda katika *Executive* utakuta Mawaziri wanaheshimiwa sana na mtu hawezi kuwagusa kwa sababu wako kule na wamejiwekea mipaka yao. Vile vile, ukienda Mahakamani unakuta Majaji wana heshima zao. Sasa, hizi *privileges* katika Bunge letu naona kuna upungufu unaosababisha mpaka wakati mwingine unakuta hata mambo yetu yanahukumiwa na Mahakama.

Mheshimiwa Spika, ninaomba vitu kama hivyo viwekwe bayana kwamba Bunge liheshimike. Tulivyo na nyumba nzuri namna hii hapa, basi na sisi wenyewe tuonekane wazuri hivyo hivyo na heshima yetu iwepo kama tulivyokubaliana katika Katiba ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kupendekeza hapa kwamba, kama lilivyo Bunge na Mbunge basi tufanane, yaani tufanane ile heshima. Mtu anapokuwa mahali popote unajua huyu ni Jaji, huyu ni Waziri na unajua huyu ni Mbunge. Kwa hiyo, tusione kwamba Mbunge ni mtu tu labda kwa sababu akiwa pale Bungeni, hapana. Hata akiwa nje ya Bunge apate heshima yake iwekwe kwenye *privileges* zetu.

Mheshimiwa Spika, hii *privilege* ni miaka mitano tu, ukimaliza miaka mitano imekwisha. Tusione tabu kumpa heshima huyu Mbunge ambaye amechaguliwa na maelfu ya Wananchi, wamem-*present.* Utakuta Mbunge anafika mahali labda anakuwa *harassed.* Sasa, anavyokuwa *harassed* kuna maelfu ya wale watu waliomchagua wanaweza wakahamaki na wakihamaki itakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, kama kuna sheria inayomlinda Mbunge na heshima yake apewe hiyo heshima.

Mheshimiwa Spika, napenda nitoe angalizo la pili kuhusu mikutano ya kwenye Majimbo yetu kwani kuna jambo linalotokea hasa katika kipindi hiki cha Vyama vingi. Wabunge wanaingia katika Majimbo ya Wabunge wengine, wanatukana matusi makubwa makubwa na hii imefanyika Tanzania nzima. Sasa, hayo nayo tunatakiwa tuyaangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria ya mwanzo inasema kwamba: “Mbunge atahutubia kwenye Jimbo lake.” Wakati ule kulikuwa hakuna Vyama vingi, sasa Vyama vingi vimekuja na visingizio kwamba: “Mimi kwa sababu ni Katibu Mwenezi Taifa, basi nitakwenda kwenye Jimbo la mwingine.” Tuiweke kwamba Mbunge kama Mbunge hata kama ana cheo hicho basi asivamie Majimbo ya wenzake na kwenda kupeleka matusi kule, kwa sababu tayari wewe una kofia ya Ubunge u-*behave* kama Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haya mambo ya adhabu. Nilikuwa nina angalizo vile vile. Sasa hivi ni wakati wa Vyama vingi vya Siasa na tuna hoja tunazokuja nazo huku na wakati mwingine hoja zinaweza zikaudhi mtu kwa sababu sisi tunapingana na Chama Tawala kwa hoja. Sasa, unaweza ukatoa hoja ikamwudhi mtu akafanya visa na baadaye akakuweka mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, ningetaka busara itawale zaidi kwa sababu sisi ndiyo kazi yetu kupingana. Unaweza ukampinga mtu ikamwudhi, akakuweka mahali pabaya. Tuangalie na hizo adhabu kwa wapinzani ni namna gani maana ni lazima tupinge na ndiyo sababu tuko hapa, lakini tupinge kwa hoja. Tukifanya namna hiyo na ikimwudhi mtu, basi hapo busara itawale kwa misingi ya kwamba ni Vyama vingi vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, kuna huu ushauri wa bendera. Nisingependa nitumie muda mwingi leo kwa sababu ni hoja ambayo inaeleweka. Lakini ndani ya Jimbo la Mbunge kama anatumia Bendera yake anakwenda kwenye mikutano yake sioni sababu ya kumwekea tena masharti, maana nimesoma mahali hapa kwamba: “Iwe ni mikutano ya kikazi.” Sasa, Mbunge ni wakati gani hana kazi ndani ya Jimbo lake?

Mheshimiwa Spika, nyumbani kwangu watu wanakuja kuanzia saa 12.00 asubuhi kunakuwa na foleni, ninaanza kazi. Nikirudi kwenye mikutano ya hadhara usiku wanakuja, nawahudumia.

Sasa, tusiweke mipaka ndani ya Jimbo lake kwa sababu ndani ya Jimbo lake anafanya kazi saa zote. Vile vile, tusiseme kwamba huu mkutano siyo wa Chama, kwani nafikiri ile bendera inatuonyesha kwamba huyu ni Mbunge na ni Mbunge wa Jimbo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na maoni kwamba si vizuri kupeperusha bendera kwenye Majimbo ya wenzako labda kama uko safarini. Pia, si vizuri kabisa kwenda na bendera kwenye Majimbo ya wenzako na kwenda kufanya mikutano yako kule kama Mbunge. Ile sheria ya zamani iwekewe meno zaidi kwamba kweli Mbunge akija kwenye Jimbo lako na akitoa matusi, basi imbane moja kwa moja mpaka huku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna mtu mmoja sitaki kumtaja jina, amekwenda amesema: "Ngawaiya amepewa Sh.1,200,000/= awaletee kwenye *supper* na sasa hajawaletea na mimi mwenyewe nakwenda Dar es Salaam kuchukua Sh.1,200,000/= napeleka kwenye Jimbo langu." Sasa, hebu fikiria matusi kama hayo, ni kweli mimi napewa Sh.1,200,000/= kupeleka kwenye Jimbo? Mimi sijui, sijawahi kupewa hizo pesa za kupeleka kwenye Jimbo! Mambo kama hayo tuyaangalie katika sheria hizi zinazolinda haki za Mbunge.

Mheshimiwa Spika, turuhusu kwamba Mbunge anapokuwa kwenye Jimbo lake atumie bendera anavyotaka mradi asitumie kama shuka, asitumie kama shati, ila aweke kwenye gari nzuri au aiweke ofisini kwake vizuri. Pia, hawa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya waelezwe kabisa kwamba hii Bendera imepitishwa kwa mujibu wa sheria. Kwa hiyo, iheshimike kama inavyoheshimika bendera ya Taifa, saa ya kupandisha, saa ya kuteremsha iwe ni wakati ule ule, wajue kabisa kwamba ni chombo kikubwa kinachostahili heshima yake.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nisitumie muda mwingi, naomba huo ushauri wangu uzingatiwe ili tuweze kufanya jambo hili liende vizuri kwa heshima ya Bunge letu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Mheshimiwa Spika, alikuwa ananichokoza rafiki yangu hapa anasema 'jazba', lakini nimemsamehe.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Muswada huu. Nilidhani tungeupata kama ile Miswada ya kawaida, lakini vinginevyo nadhani labda pengine umekuja *under certificate of urgency*, unatuhusu sisi na una kichwa cha habari ambacho kwa kweli ukikiangalia unadhani sasa hapa ndiyo mambo yanaiva maana kuna kinga, kuna madaraka na haki zote za Mbunge na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninayotaka kuchangia ni ya jumla kwamba, kama tungepata mapema, pengine na sisi tungeweza kutoa marekebisho mengine kama alivyofanya Mheshimiwa Waziri, japo na marekebisho yenyewe aliyoyatoa yamechelewa. Sasa ndiyo ilikuwa tabu hiyo kwamba huwezi ku-*time* wakati. Kwa mfano, sasa hivi nilitaka kufanya mabadiliko, lakini siwezi kufanya kwa sababu ya utaratibu ambao inabidi uzingatiwe. Katika suala hili kama tunazungumzia kinga, madaraka na haki, yapo mambo ya msingi ambayo walikuwa wanayazungumza hapa Waheshimiwa wanaotoka Kambi ya Upinzani maana sheria hii imekuwepo wakati wa Chama kimoja na wakati wa Vyama vingi.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu hii inapopita katika mfumo wa Vyama vingi na historia yake, ni bahati nzuri kwa mujibu wa historia ya nchi yetu hatuna udini, hakuna ukabila mkubwa, wala yale mambo mengine kwa kiasi ambacho watu wanakuwa *fanatic* katika hilo. Lakini bahati mbaya, nataja *with confidence* kwamba nchi hii sasa badala ya udini, ukabila na mengine inaingia katika uchama.

Mheshimiwa Spika, sasa, Chama kinakuwa ndiyo dini, kinakuwa ndiyo kabila mpaka inakwenda *to the extreme* kiasi kwamba washabiki wa eneo fulani wanawaunga mkono watu wa Chama fulani, wanakwenda hivyo na kufanya mambo ambayo kwa kweli yanakiuka haki na pengine kwa sababu hizo za uchama ambazo sasa tunazikuza na sijui zitatuelekeza wapi, tunafika mahali ambapo haki za wengine zinavunjika na yule anayezivunja hawezi kuchukuliwa hatua.

Mheshimiwa Spika, japo sikubaliani na suala la kwamba Mbunge alindwe, awe na walinzi kupita kumi, kwa sababu hata Mawaziri sijui, labda wanalindwa huko kisirisiri, lakini sijaona wanalindwa na sijawahi kusikia mmoja amedhurika. Kwa hiyo, nchi yetu ni ya amani, tunadhani hata Mbunge asipolindwa kwa maana ya kuwekewa walinzi tunaweza kuendelea vizuri, lakini taratibu za kukabiliana naye, sijui unakabiliana naye kwenye nini, taratibu zile ziwe za heshima.

Mheshimiwa Spika, ninakumbuka Mheshimiwa Ngawaiya juzi alilia kwenye Mahakama, nasikia Mahakama ilijaa machozi. Atanisamehe, lakini nadhani hatanipiga *point of order.* Alilia wakati akieleza alivyokamatwa na Polisi na kufungwa kama mbuzi. Nadhani suala hilo liko mahakamani na silipeleki kwa maana ya Mahakama. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nadhani Mbunge amechaguliwa kwanza siku moja na Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ana heshima yake kwa kikatiba na Mbunge ana heshima yake. Hata kama amekosa ukimuita aje sijui kama atatoroka, maana akitoroka ni kwamba na Ubunge auache aende. Sasa, haya mambo ya kumburuza buruza kama unaburuza mbuzi si vizuri na hakuna anayekemea na kila mmoja anacheka tu kwa sababu nadhani za uchanga wa siasa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, Mbunge anakwenda kwenye Jimbo lake, watu wanasema: "Tumesikia Mbunge anakuja, tunakuja hapa kumpokea na kumpongeza." Inatokea watu wengine hawapendi, wanaamrishana kwamba: "Huyu akamatwe, adhalilishwe" kama ilivyokuwa kwa Mheshimiwa Lwakatare.

Mheshimiwa Spika, nadhani roho wa Mungu kwa wale wanaomuamini achukue kidole chake aguse kila roho ya mtu na dhamira yake. Mbunge anakwenda kwenye Jimbo lake, wewe unaamrisha Polisi wampige, wapige na watu eti atavunja amani! Ni Mbunge gani huyo ambaye hana akili timamu? Alipojaza fomu za kugombea aliambiwa awe na akili timamu, kama hana mnamuwekea pingamizi. Sasa, eti anataka kuvunja amani kwenye Jimbo lake, sijui ana akili timamu, sijui hana! Lakini hii siioni humu.

Wewe unaamrisha dhidi ya mtu anayeunda nguzo ya tatu, tena alichaguliwa na watu, wewe sijui wamekuteua, maana umechaguliwa na Rais. Ndiyo maana hata Kanuni zetu zinasema: "Huwezi kusema maneno ya ovyo ovyo kuhusu jina la Rais au kulitumia ovyo ovyo. Sasa Mbunge wewe unatoka hapa, eti anataka kuvunja amani wala huja-*consult* mahali popote, hata Waziri wako hujamwuliza, Waziri Mkuu hujamwuliza, wewe unakaa pale kwenye Wilaya na Katiba haikutambui kwamba wewe ni mmoja wa Viongozi Wakuu wa nchi hii, kwa sababu inawatambua kwamba Viongozi Wakuu ni hawa, lakini wewe haumo. Unaamrisha Kiongozi Mkuu katika ile *protocol* akamatwe na kudhalilishwa pale bila ya kuwauliza hata wakuu wako na ukishafanya hivyo kwa sababu hizo hakuna mtu ambaye anachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira kama haya ndiyo nimesema ule uchama sasa unatuharibia. Kwa hiyo, ilikuwa inabidi tufike mahali mambo kama haya tuone kwamba hivi Mbunge akitaka kukamatwa unafanyaje? Ni bahati nzuri mimi kwangu sina ugomvi na *DC* wala *RC* na wao wananijua ni kichwa ngumu, hawawezi kuja kunikurupukia. Lakini kuna watu wanalalamika kwamba kuna watu, sijui *DC*, sijui nani anakwenda anavuruga. Mbunge amesema hivi na yeye anajipitisha pale anaanza kusema mambo yake mengine, huenda pengine labda na yeye anakuwa anategemea kugombea, lakini bahati nzuri kwangu hawajafanya hivyo. Lakini tunapokuwa tunazungumza na wengine kitu kama hicho kipo, kwa makusudi mtu anakwenda pale anataka kuhujumu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mbunge akikosea kama watu wengine *okay,* yapo mambo mengine ambayo labda ni ya hatari zaidi alitaka kufanya. Tukiwa tunaingia humu ndani ya Bunge huwa wanatukagua. Juzi niliuliza: "Hivi huyu Mbunge anaweza kutaka kwenda kulipua humu ndani?" Nadhani na wao wamechoshwa. *Anyway,* lakini ni utaratibu ambao mmefanya. Labda Mbunge anaweza kusababisha hatari katika mazingira hayo akakamatwa kwa ghafla, lakini kama yako mambo mengine ni lazima tuwe na *authority,* tujue kwamba huyu Mbunge kama yuko kule Kyerwa, kama yuko kule Mtwara na tunadhani lazima achukuliwe hatua tufuate utaratibu, lakini siyo unakwenda unamkamata kama unakamata mbuzi.

Mheshimiwa Spika, kipo kitu kimesemwa hapa na sitaki kuendeleza mjadala katika hili na sitaki kuchelewesha Bunge lako, lakini nadhani kwa ajili ya *record* tufanye hivi: Katika Bajeti ya mwaka huu Wabunge wa Kambi ya Upinzani kwanza kwa aliyewawakilisha hapa kuhusu bajeti na wote kwa pamoja waliunga mkono Bajeti ya Serikali na wote tulishangilia hapa, ninyi mkisema 'CCM' sisi tunasema 'Wapinzani' iko kwenye *record.* Kwa hiyo, Wabunge wa Kambi ya Upinzani hawawezi wakakaa wakamwonea mtu kwamba aliunga mkono Bajeti hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunajua kwamba humu tunafuata Itikadi ya Chama chako, Jimbo lako limekutumaje, dhamira yako inasemaje. Mimi ni miongoni mwa watu ambao ningependa sana kama si hizi sheria, kuhakikisha kwamba *I express what I feel.*

Nakumbuka *Galiley* aliwahi kusema: *"A man convicted against his will, he is still of the same opinion."* Anawaambia wale watu wa Kanisa ambao walikuwa hawataki kuelewa kwamba: "Dunia ni mviringo." Wakasema: "Hapana. Kwanza, Biblia inasema Mungu alisimamisha jua, sasa wewe unaleta hapa unakufuru tutakutoboa macho." Lakini akawaambia: "Hata kama mkiyatoboa, ukweli unabaki kuwa ndiyo huo huo." Kwa hiyo, nina uhakika kwamba mtu anayo haki ya ku-*express views* zake vile anavyoona, pamoja na kwamba sheria hizi zinatulinda. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini yapo mambo ya msingi ambayo pengine ndiyo unakuwa ni ugomvi. Nilipokuwa naunga mkono Maazimio nilisema: "Naunga mkono kwa niaba ya Kambi." Sidhani kama kuna mtu ataniuliza kwamba: "Kwa nini ulisema hivyo? Pia, Mheshimiwa hapa ameunga mkono. Kwa hiyo, hiyo si hoja katika mambo ambayo alikuwa anayasema Mheshimiwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, uji wa mahindi kwa kweli ni unga wa mahindi uliowekwa katika maji yaliyochemka kwa *centigrade* nadhani 100 na ugali wa mahindi ni unga wa mahindi uliowekwa katika maji yaliyochemka kwa asilimia 100, lakini yana majina tofauti kwamba, huu ni uji na huu ni ugali. Nadhani kuna *point* moja ya msingi ndiyo maana huu ni uji na huu ni ugali. *(Makofi)*

Sasa, katika hiyo ya kwamba aliunga mkono sijui ikawaje, yapo mambo mengine ya msingi. Kwa hiyo, nadhani hoja hapa siyo wanamwonea mtu fulani, zipo hoja zitakuwa kwa Spika huko, nadhani watazijadili na wataona mwisho wake inakwendaje kwa sababu naamini kila Mbunge ni Mbunge anapokuwa hapa na ana haki zote za Ubunge. Yale mambo yanayojitokeza yapo na yatatatuliwa kwa msingi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru. Walikuwa wananidokeza hapa, lakini nadhani niliache. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru sana Waheshimiwa waliochangia hoja hii nikianza na Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Eliachim J. Simpasa. Lakini pia naomba kumtambua Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kwa michango yao. Vile vile, naomba kumtambua Mheshimiwa Philip S. Marmo, ambaye amechangia vizuri. Lakini pia naomba kumtambua Mheshimiwa Thomas Ngawaiya na mwisho Mheshimiwa Benedicto M. Mutungirehi. Kwa ufupi wote wameunga mkono hoja hizi, lakini nitakwenda kwa ufupi juu ya hoja zenyewe nikianza na Mheshimiwa Mwenyekiti. Kwa kuwa tulikuwa wote kwenye Kamati na mengi waliyokuwa wamependekeza tumeyarekebisha, isipokuwa kuna moja tu naona alikuwa anaweka mashaka. Anauliza kuhusu wale watu wanaofanya fujo kwenye ile mikutano kwani Sheria Mama kifungu cha nne kinasema kwamba ni kosa kuzuia au kuingilia mikutano; je, adhabu iko wapi?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika marekebisho haya utakuta tumefanya marekebisho kidogo katika sheria ile ile namba 4 ya Sheria Mama na tumeweka adhabu sasa kwamba itakuwa faini ya Sh.100,000/= au kifungo kisichozidi miaka mitatu. Kwa hiyo, hilo jambo ambalo alikuwa anasema Mwenyekiti tumeliweka vizuri na tunashukuru sana kwamba Kamati tumeshirikiana nao vizuri. Nataka niwaambie hii si sheria mpya maana Mheshimiwa Mutungirehi anauliza imekujaje? Hii ni sheria ambayo ipo tangu 1988. Tumekuwa na tabia ya kufanya marekebisho, haya ni marekebisho machache tu tumeyafanya na tumekubaliana wenyewe tangu Bunge lililopita na kwenye kanuni tumeishaingiza na tutaendelea kufanya marekebisho kulingana na wakati kwa sababu sheria hii haiwezi kuganda.

Mheshimiwa Spika, maoni ya Mheshimiwa Mwenyekiti yanaungana na maoni ya Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed kwamba, tuangalie kwa baadaye, kwa sasa tumeishakubaliana wote mpaka kwenye kanuni tumeweka kwamba bendera zitapeperushwa isipokuwa katika Mji wa Dar es Salaam na siyo Zanzibar. Mheshimiwa Hamad, ni Manispaa ya Zanzibar wala si Pemba, si Kusini Unguja wala Kaskazini Unguja, ni Manispaa pale. Wengine wanafikiri kwamba kwa sababu Manispaa ipo katikati,

itakuwa kila mara ukikatisha lazima utungue ile bendera na upandishe. Kwa hiyo, unajikuta kama umepigwa marufuku Zanzibar nzima. Ni Manispaa ya Zanzibar tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hilo tumekubaliana katika Kamati na tumekiri kwamba tutaendelea kulifanyia utafiti ili tuone hata wenzetu hawa wa Dar es Salaam, Dodoma na Manispaa ya Zanzibar inakuwaje. Lakini kwa leo ningeomba Waheshimiwa Wabunge tukubaliane na haya tuliyoyaweka kwenye Kanuni. Ndiyo tunaanza, hizi *restrictions* za Dar es Salaam, Zanzibar na Dodoma tuanze nazo. Tutapata uzoefu tutakuja tena. Hii Kamati ina Waheshimiwa Wabunge humu humu, haya yote mimi nasoma tu, lakini yamejadiliwa kwenye Kamati yenu wenyewe. Mie niko hapa nawawakilisha tu. Kwa hiyo, tutaangalia uzoefu wetu unatuonyesha nini juu ya Dar es Salaam, Dodoma na Manispaa ya Zanzibar. Vile vile, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed amezungumzia juu ya kuchukua uzoefu wa Zanzibar kuhusu *immunities,* wenzetu wamekwenda zaidi kidogo. Tumepokea ushauri huo na tutajifunza, maana hata hili la Bendera ilibidi twende tukaulize kule wenzetu hivi mnapeperushaje huku? Wakasema: "Sisi hatuzuiliwi, hata Mawaziri nao wana Benderara zao." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza tukapeperusha, lakini aina tu ya kisiwa chenyewe kilivyo, baada ya dakika 10 unaweza kujikuta umeishakwenda mpaka mwingine umeshaingia Manispaa na kazi zao nyingi wanafanyia pale Manispaa. Kwa hiyo, wanajikuta tu hawawezi kupeperusha bendera, lakini siyo kwamba wanazuiliwa kupeperusha bendera nje ya Manispaa ya Zanzibar. Kwa hiyo, tutajifunza tuone hizo immunities nyingine zikoje, zitapelekwa kwenye vikao vinavyohusika, tutazijadilli wote, tutaona kama zinaweza zikatusaidia. Wanauliza kwa nini bendera hizi zisitumike katika shughuli zote za kisiasa? Hizi zinaruhusiwa, tunaweka kwenye ofisi zetu, tunaweka kwenye magari na magari haya hayana mipaka. Tumesema likiwa kwenye *highway* hata kama ni Mbunge wa Mafia anakwenda Iringa, kwenye *highway* anapita.Katika hili napenda nimweleze Mheshimiwa Ngawaiya kwamba, Mbunge yeyote ni Mbunge wa Kitaifa, hana mpaka. Kwa hiyo, hawezi kuja Moshi Vijijini akafungua bendera, isipokuwa *restrictions* zilizowekwa hapa kwamba akiwa Dodoma, Zanzibar na Dar es Salaam. Haiwezekani Mbunge anakatisha pale Moshi Vijijini katika Jimbo la Mheshimiwa Ngawaiya anateremsha bendera, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Janet Kahama, naomba nikutambue. Umechangia kwa maandishi na unauliza Wabunge wa Viti Maalum vipi? Hapa hakuna utengano, sheria hii inatugusa wote. Mbunge wa Viti Maalum hutapandisha bendera ukiwa tu pale Dar es Salaam, Dodoma na Zanzibar, kwingine kote, hata ukija Ismani, Iringa na mimi nikiwa kule kule tutakuwa na bendera mbili, haina matatizo. Mheshimiwa Marmo, kwa uzoefu wake ametukumbusha mengi sisi wote, Waandishi wa Habari pamoja na Wananchi kwamba, kwa bendera hizi sisi Wabunge tusionekane tunaomba kama mbwembwe, hapana. Tumechelewa sana ni haki yetu. Ninakubaliana naye sana.

Yale mengine aliyotoa ushauri tunayaafiki na tunakubali kwamba hata sisi tumeona kuwa wakati umefika wa kuwa na hizi Kanuni za Maadili ambazo zitachambua na kuweka maadili mazuri kwa ajili ya shughuli zetu na nashukuru kwamba sheria hii inazitambua tayari hizo Kanuni za Maadili. Pia, ameunga mkono kile kifungu cha 10 kinachokataza Mbunge kununuliwa nunuliwa tu, kutumwatumwa tu kuja kuleta mahoja hapa huyajui ili mradi tu umeahidiwa jambo fulani. Sasa, adhabu iko hapa. "Ooh, bajeti hii mzee kanisemee, mafuta haya yashushwe" kumbe una *10 percent.* Hapa umekamatwa. Kwa hiyo, tunakubaliana na maoni ya Mheshimiwa Marmo na ndiyo maana tumeweka hapa. Mengine alikuwa anaelezea tu, anatoa ufafanuzi kwa sababu yeye alikuwepo kipindi chote tangu kanuni hizi zimeanza kutumika. *(Makofi)*

Kuhusu *issue* ya Mheshimiwa Ngede, nafikiri jana Kamati ya Uongozi tumelimaliza chini ya Mheshimiwa Spika na Kiongozi wa Upinzani alikuwepo. Tumekubaliana kwamba, sisi kama Bunge tunaamini kuwa Mbunge ni Mbunge na anazo haki zote ndani ya Bunge hili. Kwa hiyo, kama kuna mambo mengine sisi hatuna uwezo kama Bunge kumnyima mtu nafasi anayotaka kugombea ambayo iko chini ya utaratibu wa kanuni na utaratibu wa Bunge. Sisi tulimwomba na tulimsihi mwenzetu Kiongozi wa Upinzani awaarifu wenzetu na ninafikiri Mheshimiwa Spika amewajibu kwamba kwetu sisi ndani ya Bunge wote ni sawa sawa na tuna haki sawa.

Mheshimiwa Spika, nafasi ilitolewa wagombea watatu wakajaza fomu ila nasikia mmoja amejitoa. Mheshimiwa Cheyo alijaza fomu, lakini baadaye alijitoa. Hata hivyo, tunayemtaka ni mmoja, lakini huu ni

uungwana na umefanywa na Bunge. Kinachotakiwa ni kwamba, tuwe na Tume yenye Wajumbe ambao ni Wabunge. Uungwana wa Bunge hili ndiyo ukafanya mgawanyo huo, jamani tuonyeshe *solidarity* tuwe na mama mmoja, tuwe na mpinzani na tuwe hivi. Ni uungwana tu. Kwa hiyo, sisi tunajua kwa vyovyote tukifanya uchaguzi ni lazima tutampata mpinzani kwenye Tume. Sasa ni nani? Ni miongoni mwa hao walioomba maana hii ni nafasi ya kuomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema tu kwa sababu Mheshimiwa Marmo alichangia hapa kidogo, natoa taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Hata akiwa ni mwanamke?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Eeeh.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ngawaiya anasema tuheshimu hizi *pillars* tatu na kweli zinaheshimika kwa mujibu wa Katiba na zinatambulika na Wananchi wote wanajua hiyo mipaka. Pia, anasema *privileges* za Mbunge zina upungufu kidogo na heshima ya Mbunge iwepo kila mahali. Vile vile, hii ameirudia Mheshimiwa Mutungirehi, akifananisha jinsi Polisi walivyomfanyia Mheshimiwa Ngawaiya na pia amezungumzia juu ya yaliyompata Mheshimiwa Lwakatare kule Bukoba.

Mheshimiwa Spika, *privileges* za Mbunge zipo na zimeainishwa vizuri katika sheria yetu na sheria nyingine, lakini tunasema Mbunge katika Jamhuri hii ni raia kama raia wengine, anatakiwa atii na sheria nyingine za nchi. Kwa hiyo, kama Mbunge, hatakuwa na fursa ya kuvunja sheria nyingine zilizopo. Yaliyompata Bukoba Mheshimiwa Lwakatare mngemwuliza, yeye anayajua na amekiri na mambo yameisha kwa sababu upo utaratibu wa yale aliyotaka kuyafanya. Mbunge ni kiongozi, *yes,* lakini ukitaka kufanya hizo mbwembwe alizotaka kufanya Mheshimiwa Lwakatare kuna utaratibu. Ni lazima ufuate utaratibu, uruhusiwe, watu wajipange kukusaidia utekeleze vizuri ule utaratibu ulioutaka ili uweze kutekeleza. Jambo hili sitaki kumsemea Mheshimiwa Lwakatare, kwa sababu hayupo, lakini mwenyewe analijua na mambo yote yako shwari, wala si tatizo tena.

**MBUNGE FULANI:** Ugoni je?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, wananiuliza hapa kwamba; je, hata ukikamatwa ugoni mpaka *AG* aseme kwamba asikamatwe? Sasa, yapo mengine ambayo yanalindwa na sheria zilizopo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Ngawaiya amezungumzia habari ya Wabunge kuingilia Majimbo ya watu wengine. Sina ushahidi wa haya anayoyasema na sijui alikuwa anamlenga nani, lakini kwa sababu yeye hakutaja na mimi sitaki kutaja. Sasa, labda baadaye hizi Kanuni za Maadili tutakazoziweka tutajuana wenyewe. Kiungwana tuliishasema kwamba, Mbunge akitaka kutembelea Jimbo la mwenzake Tuambizane. Lakini sasa kwa sababu tunazitambua hizi Kanuni za Maadili tutakaa, tutazungumza tuwekeane *Code of Conducts* tujuane.

Mheshimiwa Ngawaiya, najua umeshindwa kusema kwa sababu wengi wanaofanya hivyo, wanaotukanatukana wanatoka kwenye Kambi yako ndiyo maana umeshindwa kusema. Wanakutukana hata wewe nasikia. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mu-*address* Spika.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Ooh, ndiyo. Nashukuru. Nilikuwa naunga mkono hoja ya yule Mheshimiwa ili awaambie, nafikiri alikuwa anawapa *message* wenzake. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mbunge ndani ya Jimbo lake asipewe masharti ya bendera. Hii ni hoja ya Mheshimiwa Ngawaiya, hakuna masharti. Nimesema na ninarudia tena. *Restrictions* zipo kwenye yale maeneo ya Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar. Bendera yako ya gari utakwenda nayo kila mahali hata kwenye mkutano nenda nayo. ile ya mezani itakuwa ofisini au mahali popote ulipo. Hata kama unataka

kuhutubia mkutano pale kuna meza, chukua kale kabendera kako beba weka pale. Lakini ambacho hatukuweka hapa ni kwamba ile bendera, zile za mbwembwe mnatundika kwenye miembe, tusingependa bendera yetu itundikwe kwenye miembe.

Mheshimiwa Ngawaiya, kwa mfano unahutubia na bendera iko juu kwenye mwembe, hapana, tutaishushia hadhi kidogo. Lakini ya gari haina mipaka. Baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria wa Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya Mwaka 1988 wa Mwaka 2004 usomwe mara ya pili.

*(Hoja liamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge wa mwaka 1988 wa Mwaka 2004.** ***(The Parliamentary, Immunities, Powers and Privileges Amendment) Bill, 2004)***

Kifungu cha 1

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 2

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Kifungu cha 3

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 4
Kifungu cha 5
Kifungu cha 6
Kifungu cha 7

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Kifungu cha 8
Kifungu cha 9

*Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho)*

Kifungu cha 10
Kifungu cha 11
Kifungu cha 12

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

Jedwali

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya mwaka 1988 wa Mwaka 2004.** ***(The Parliamentary, Immunities, Powers and Privileges (Amendment) Bill, 2004)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya Kufanya Marekebisho katika Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya mwaka 1988 wa mwaka 2004 *(The Parliamentary, Immunities, Powers and Privileges Amended Bill, 2004)* ukubaliwe na kupitishwa na Bunge lako tukufu. Naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokwishaeleza mpaka hapo tumefikia mwisho wa shughuli zilizopangwa kwa ajili ya Kikao cha leo. Kama nilivyoeleza tunahitaji nafasi kwa ajili ya kupamba Ukumbi huu, kwa ajili ya kuupokea ugeni mzito wa kesho. Kwa hiyo, sasa naahirisha Bunge mpaka kesho Asubuhi Saa Tatu.

*(Saa 06.33 mchana Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi*
*Tarehe 12 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*